**MAUDHUI YA UBAGUZI KATIKA *MHANGA NAFSI YANGU***

**NA**

**MUSYOKI CAROLINE NDUKU**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2016**

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya kutosheleza shahada ya uzamili katika chuo kikuu kingine.

……………………………………… ……………………………………

**Caroline N. Musyoki** Tarehe

**(Mtahiniwa)**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

……………………………………… ……………………………………

**Prof. Mwenda Mbatiah** Tarehe

**(Msimamizi)**

……………………………………… ……………………………………

**Dkt. Zaja Omboga** **Tarehe**

**(Msimamizi)**

**TABARUKU**

Tasnifu hii nawatabarukia wazazi wangu Bw. Nicholus Musyoki na Bi. Philomena Syombua walionilea na kunisomesha na kunifanya niwe na kiu ya masomo.

Vilevile, namtabarukia bwanangu mpenzi, Salaton Naikuni ambaye amekuwa mhimili mkubwa katika masomo yangu.

## SHUKRANI

Ukamilifu wa tasnifu hii haungekamilika pasipo na mchango wa watu mbalimbali. Kwa Mola muumba wangu, ni mkono wa tahania kwa kuniongoza kutoka mwanzo hadi sasa.

Shukrani za dhati na maalum ni kwa wasimamizi wangu Prof. Mwenda Mbatiah na Dkt. Zaja Omboga. Hawa wamekuwa wasimamizi wa kupigiwa mfano.Ushauri wao umeufanikisha utafiti huu. Mola awe nanyi siku zote za maisha yenu.

Shukrani zingine nazitoa kwa wahadhiri wangu wengine katika idara ya Kiswahili katika Chuo kikuu cha Nairobi ambao walinisaidia na kunielekeza katika kazi hii ya usomi. Hawa ni: Prof. John Habwe, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Iribe Mwangi, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Amiri Swaleh, na Dkt. Jerono. Mwongozo na ushauri wenu ulinifaa pakubwa. Mola awe dira siku zote za maisha yenu.

Kama si wewe mume wangu Naikuni, chombo changu kingeenda mrama. Ulinihimiza na kunisaidia nilipokuhitaji hasa kifedha na motisha ya kuendeleza masomo yangu. Wewe umekuwa mwelekezi mkuu katika maisha yangu. Wanangu Rakita na Naini mlivumilia kwa kutokuwa nanyi mliponihitaji. Langu sasa ni kuwaombea baraka na neema zake Mola ziwe nanyi siku zote.

Sitowasahau wanafunzi wenzangu: Winnie, Kihara, Kimetto, Kelvin, JohnBosco, Asha, Emmily, Kimeu, Jacklyn, Mangistu, Meshack, Silveria, Chesebe, Zahra, Wangeci, Faith, Waweru, Chepkorir, Bi.Gitonga, Xariun, Lydia, Mogusu, Bosibori, Jared, Kemunto, Lilian Anyango na Polycap Adika. Nawashukuru kwa dhati ya moyo wangu, Mungu awajalie neema yake mnapopanda ngazi hii ya masomo.

Namshehenezea shukrani mwalimu mkuu wa shule ya Matungulu Bw. Matheka. Ulinielewa na kunisaidia kila nilipotaka kwenda katika shughuli za masomo haya. Neema ya Mola iwe nawe siku zote.

Nawashukuru wote waliohusika kwa hali yoyote ile, mlikuwa msaada kwangu. Japo sikuwataja kwa majina, nasema asanteni sana na Mungu awabariki.

**IKISIRI**

Tumeangazia Ubaguzi katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ya Said.A Mohamed. Tulichagua mada ya ubaguzi katika riwaya kwa sababu swala hili linatokea katika riwaya nzima ya *Mhanga Nafsi yangu*, na ni wajibu wetu kuwahamasisha Waafrika uhalisia wa mambo wanapohamia Peponi. Hii ni kwa sababu jamii zetu za Kiafrika zinahusudu Peponi kana kwamba hakuna shida zozote zipatikanazo huko na kuona kuwa watapata suluhu ya shida wanazokumbana nazo huko. Tulilenga vilevile kuchunguza changamoto zinazowakabili Waafrika Peponi na kuwazuia katika juhudi zao za kujikomboa kutoka katika matatizo mengi kama vile umasikini. Aidha ubinafsi, dhuluma, utabaka uliokithiri na ubaguzi ni baadhi tu ya changamoto wanazokumbana nazo Waafrika Peponi.Utafiti wetu umeongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu tukijikita katika kiunzi chake kinachodai kuwa Uhalisiajabu hueleza kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu ambapo uhalisi na ndoto, kifo na uhai, usasa na uzamani, shamba na mjini, ugeni na wenyeji huingiliana kiasi kwamba mpaka uliopo baina ya hali hizi ni mdogo sana. Mwongozo huo umetufanya kuitathmini jamii mwanzo kabla ya kuutalii ubaguzi katika riwaya husika. Kutokana na utafiti wetu, imebainika kuwa Said.A Mohammed amefaulu katika kuisawiri jamii ya Waafrika inavyobaguliwa na jamii ya Wapeponi na asasi zinazoendeleza ubaguzi kama vile sheria, ndoa, polisi, na pia elimu Aidha mwandishi ametoa mchango wake muhimu katika kuwajenga wanaobaguliwa kihadhi.

## YALIYOMO

**Ungamo ........................................................................................................ i**

**Kutabaruku ........................................................................................................ ii**

**Shukrani........................................................................................................ iii**

**Ikisiri ........................................................................................................ iv**

## SURA YA KWANZA

1. 1 Utangulizi........................................................... **Error! Bookmark not defined.**

1. 2 Tatizo la Utafiti ........................................................................................ 3

1 .3 Malengo ya Utafiti ........................................................................................ 4

1. 4 Maswali ya Utafiti........................................................................................ 4

1. 5 Sababu za kuchagua mada ........................................................................................ 4

1. 6 Upeo na Mipaka ya Utafiti........................................................................................ 5

1. 7 Msingi wa Nadharia ........................................................................................ 6

1. 8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada........................................................................................ 14

1. 9 Mbinu za Utafiti ........................................................................................ 20

**SURA YA PILI**

**TATHMINI YA HALI YA JAMII KATIKA *MHANGA NAFSI YANGU***

2. 1 Utangulizi....................................................................................................21

2. 2 Riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* kwa muhtasari .................................................22

2. 3 Uhalisiajabu katika riwaya ya *mhanga nafsi yangu* ............................................29

2. 4 Sababu za kuhamia Peponi ....................................................................................42

2. 5 Manufaa ya kuhamia Peponi..................................................................................43

2. 6 Madhara ya kuhamia Peponi..................................................................................44

2 .7 Sababu za ubaguzi.................................................................................................47

2 . 8Madhara ya ubaguzi...............................................................................................48

2 . 9 Hitimisho...............................................................................................................51

## SURA YA TATU

**MASUALA YANAYOWAATHIRI WANAOBAGULIWA KATIKA RIWAYA YA *MHANGA NAFSI YANGU***

3. 1 Utangulizi....................................................................................................53

3. 2 Magonjwa sugu yanayochangia ubaguzi .............................................................53

3. 3 Ndoa za kigeni zinavyoathiriwa na ubaguzi .........................................................55

3. 4 Haki zinazopeanwa kwa ubaguzi..........................................................................57

3. 5 Sheria ....................................................................................................................60

3. 6 Mitazamo isiyo na ukweli ya Wamotoni kuhusu Peponi.....................................62

3. 7 Dawa za kulevya ..................................................................................................65

3. 8 Hitimisho..............................................................................................................66

**SURA YA NNE**

## HITIMISHO

4. 1 Utangulizi.......................................................................................................67

4. 2 Muhtasari .......................................................................................................67

4. 3 Matokeo ya utafiti..........................................................................................68

4. 4 Mchango wa utafiti .......................................................................................69

4. 6  Matatizo ya utafiti.........................................................................................70

4. 7 Mapendekezo .................................................................................................70

4. 7 Marejeleo .......................................................................................................71

# SURA YA KWANZA

## 1.1 UTANGULIZI

Utafiti huu umeshughulikia maudhui ya ubaguzi katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ya Said A. Mohamed. Ubaguzi katika muktadha tulioshughulikia ni ile hali ya watu wa nchi, tamaduni, kikundi, dini au hata rangi fulani kujiona bora zaidi au duni zaidi wakilinganishwa na wenzao wanaotofautiana kwa misingi hii. (maoni yangu). **U**baguzi pia ni hali ya upendeleo katika kuwahudumia watu. Kuna visa vingi vya ubaguzi katika jamii. Njogu (2007) anaeleza kuwa ubaguzi wa rangi ni kitendo cha kumtenga binadamu kwa misingi ya rangi yake. Tunashuhudia visa vingi vya ubaguzi wa rangi katika jamii yetu..

Katika jamii ya Kiafrika, maswala ya ubaguzi pia yanajitokeza, Katika *Nyota Ya Rehema* (1976) ya Mohammed S. Mohammed, Rehema mtoto wa Fuad anabaguliwa kwa sababu ni mweusi na tena mwanamke na haelimishwi, huku ndugu zake Samir na Salma wanaochukua rangi ya baba yao wakipewa elimu nzuri. Pia, babake na mamake wa kambo Adila, wanambagua kwa sababu ya weusi na anaamua kutoroka na kwenda mjini kuingilia ukahaba kuliko kutukanwa na kufedheheshwa.

Sigelman Lee na Susan Welch (1994) katika kitabu chao *Black Americans View on racial inequality* pia wameeleza maoni ya Wamerikani weusi kuhusu chanzo cha ubaguzi wa rangi kutokana na wenzao weupe. Katika kitabu hiki chao, inadhihirika wazi kuwa waafrika wanadhulumiwa hata kazini na kulipwa mishahara duni kuliko wenzao weupe. Pia, asasi mbalimbali kama za kijamii vile elimu, dini na ndoa zinatumika kumbagua Mmerikani mweusi. Ubaguzi wa rangi husababishwa na mambo kama kasumba za kimagharibi kwamba Waafrika ni wajinga na hakuna chochote kizuri kinachoweza kutoka Afrika. Wamerikani huchukulia kuwa elimu bora, lugha bora, siasa bora na hata teknolojia ni ile ya mataifa ya Magharibi. Hali hii ya

kujiona bora kuliko wenzao wa Kiafrika inasababisha ubaguzi. Hata hivyo, ubaguzi huu una suluhu ambapo elimu, dini na vyombo vya habari vinaweza kutumika kuondoa kasumba hizi.

Tumekubaliana na Mwita (2005) anayesema kuwa, kutokana na mfumo wa kuumeni uliokithiri katika jamii ya Wakuria, hali halisi ya mwanamke inaonekana iliyojaa ubaguzi, dhuluma, unyanyasaji na unyonyaji. Mwanamke daima anabaguliwa. Hali zote za maisha yake hutegemea uamuzi wa mwanamume. Kujiamulia mambo kwa wanawake katika jamii hiyo ni sifa hasi. Anatamatisha kwa kusema kuwa hali hii ni yakini katika jamii nyingi za Kiafrika.
Tunakubaliana naye ila kipindi tulicho nacho kwa sasa hali imebadilika. Kipindi cha miaka ya nyuma hali ilikuwa jinsi Mwita anavyoeleza. Mabadiliko tunayoyashuhudia sasa yameletwa na maendeleo ya elimu ya mtoto msichana na uhamasishaji unaoendelezwa na wanaharakati wakisaidiana na baadhi ya wafuasi wa madhehebu ya kikristo. Pia mashirika yasiyo ya kiserikali yametoa na yanaendelea kutoa mchango kuhusu uhamasishaji wa umma juu ya maswala yanayohusu ubaguzi wa kijinsia.

Ubaguzi wa rangi hasa kwa jinsia ya kike ndio swala tawala katika *Mhanga nafsi yangu*. Wanawake weusi ndio wanaoathirika zaidi na ubaguzi huu. Katika riwaya hii, aina hizi mbili za ubaguzi; ubaguzi wa rangi na ubaguzi wa kijinsia zinaingiliana hivi kwamba, anayebaguliwa ni mwanamke mweusi. Kwa hivyo, aina hizi mbili za ubaguzi ndizo tutakazochunguza katika *Mhanga Nafsi Yangu*.

Katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu,* yumo Afida ambaye anaikimbia nchi na watu wake na kwenda kutafuta maisha peponi. Safari yake imejaa matumaini lakini yanakatizwa mara tu anapofika peponi. Mazingira ya peponi na fikra mbaya walizonazo wenyeji kuhusu wageni, hasa wageni weusi, yanaonekana kuwa ni mazingira ya ubaguzi na udhalilishaji. Ubaguzi wowote ule uwe ni kwa misingi ya rangi, tabaka, asili au lugha huwaathiri watu kisaikolojia, kitabia, kitamaduni na kimaadili. Athari hizi huwasukuma kuyakubali mabadiliko mengi ilimradi wakubalike katika jamii husika. Afida na rafikiye Shuhuda walikengeuka na kuasi maadili na utamaduni wa Kiafrika, ili wakubalike katika utamaduni mpya wa Ulaya, jambo lililopelekea kukatizwa kwa ndoto zao za kujiendeleza kimaisha na kusababisha vifo vyao. Waafrika

wanakimbia nyumbani na kuhamia Ulaya wanakobaguliwa kwani huwa wanasukumwa na baadhi ya mambo yafuatayo. Umasikini, kutafuta elimu, uhitaji wa kazi, kutafuta viza na kuanza maisha mapya. Kwa ufupi, kazi yetu ilichunguza ubaguzi wa rangi unaoegemea sana kwenye jinsia ya kike katika *Mhanga Nafsi Yangu*.

## 1.2 TATIZO LA UTAFITI

Utafiti huu basi ni jaribio la kulichunguza suala hili la ubaguzi katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ya Said A. Mohamed. Kuliziba pengo hili, utafiti huu ulinuia kuchunguza ubaguzi unavyotekelezwa, kubainisha madhara yake pamoja na suluhu zake katika *Mhanga Nafsi Yangu*. Tulitumia misingi ya nadharia ya Uhalisiajabu katika uchunguzi wetu. Hivyo basi, ubaguzi wa kirangi pamoja na ubaguzi wa kijinsia utachunguzwa.

Kwa muda mrefu, mwanamke amekuwa akidhalilishwa na kukandamizwa na asasi za kijamii kama ndoa, elimu, siasa, utamaduni na hata uchumi. Kutokana na hili, utafiti huu unalenga kuchunguza namna mwanamke ameathirika kutokana na dhuluma ya ubaguzi anapohamia ughaibuni.

Ubaguzi unaojitokeza katika *Mhanga Nafsi Yangu* ni kwa Waafrika waliohamia Peponi, hii inaonyesha kuwa kuna mshawasha wa kutaka kuhamia Peponi kwa Waafrika.

Japo tafiti nyingi zimewahi kufanywa kuhusu ubaguzi kwa kutumia nadharia mbalimbali, tafiti zenyewe zimeegemea kwenye ubaguzi wa kijinsia pekee ilhali katika utafiti wetu tumejumuisha ubaguzi wa kijinsia na ubaguzi wa rangi. Ni katika utambuzi huo wa kuwepo kwa pengo hilo la kiusomi ndiposa tukaamua kuchunguza ubaguzi wa kijinsia na kirangi.

## 1.3 MALENGO YA UTAFITI.

Lengo letu la kimsingi katika utafiti huu ni kuchunguza swala la ubaguzi katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* kwa kutumia nadharia ya uhalisiajabu kwa madhumuni yafuatayo.

i. Kuchunguza swala la ubaguzi wa kijinsia na kirangi,
ii. Kubainisha jinsi Waafrika wanavyobaguliwa na Wapeponi na sababu zake.

iii. Kuchunguza kwa kina sababu za Waafrika kuhamia Peponi.

## 1.4 MASWALI YA UTAFITI

(i) Kuna ubaguzi wa kijinsia na kirangi?

(ii) Ni watu gani wanaobaguliwa, na nani na kwa misingi gani?

(ii) Ni nini kinachopelekea Waafrika wengi kuhamia Peponi?

## 1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA.

Tulihiari kuchagua mada hii ya ubaguzi kwa sababu, maisha ya Mwafrika Ughaibuni yamekumbwa na matatizo yanayotokana na ubaguzi. Ubaguzi ni swala ambalo ni hatia katika katiba yetu ya Kenya na pia katiba yenyewe inatambua haki ya kibinadamu ya usawa. Ubaguzi unaojitokeza katika *Mhanga Nafsi Yangu* unakiuka haki za kibinadamu na kuwadhalilisha wanaobaguliwa. Kazi hii basi inachunguza jinsi ubaguzi unavyoendelezwa katika riwaya hii kwani hali hii inazua changamoto nyingi hasa kwa mhusika mkuu na mwenzake ambao wanaathirika pakubwa na ubaguzi unaopelekea hatima yao.

Kwa kudurusu kazi zilizofanywa na watafiti wengine kuhusu ubaguzi, ilibainika kuwa hakuna mtu mwingine ameushughulikia ubaguzi katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* kwa kutumia mihimili ya Uhalisiajabu. Kwa hivyo, kazi yetu itawafaidi sana wasomaji wa Kiswahili. Ni matumaini yetu kuwa uchanganuzi wetu utakuwa kama changamoto kwa changanuzi fuatilizi.

Tulinuia kuwahamasisha Waafrika wasikubali kubaguliwa kwani watu wote ni sawa licha ya kasumba zinazoenezwa kuwa Waafrika ni watu duni. Mada hii itafaa sana hasa kwa wakati huu ambapo swala la ubaguzi na dhuluma kwa wanyonge hasa wanawake linapigwa darubini ili kusitishwa kote ulimwenguni.

Mtazamo wa mwandishi pia kuhusu ubaguzi wa kirangi na kijinsia katika mataifa ya Magharibi na uhusiano wao na ulimwengu wa tatu hususan bara la Afrika umetuchochea kuchagua mada hii. Katika baadhi ya kazi zake kama vile *Utengano* (1980), na *Nyuso za Mwanamke* (2010), Said A. Mohammed amezungumzia ubaguzi wa jinsia ya kike ambapo asasi nyingi kama vile dini, elimu, tamaduni na ndoa hutumika katika ubaguzi huu, kwa hivyo, tunataka kujua iwapo baadhi ya asasi hizi zitatumika katika ubaguzi unaopatikana katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*.

**1.6 UPEO NA MIPAKA.**

Kuna aina nyingi za ubaguzi ukiwepo wa kikabila, kijinsia, kirangi, kitabaka, kidini na pia ubaguzi wa walemavu. Hata hivyo, uchunguzi wetu umefungamanishwa na ubaguzi wa kirangi na kijinsia katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu.* Tulijikita kwenye riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* tu bila kujihusisha na riwaya zingine. Maudhui yanayohusiana na ubaguzi pia yalihusishwa. Japo kuna ubaguzi kote ulimwenguni, uchunguzi wetu umejikita Peponi na kubainisha maisha ya Mwafrika hasa mwanamke katika nchi hiyo ambayo ni mojawapo ya nchi za Magharibi. Tumebainisha kuwa Waafrika hubaguliwa Peponi na wanaoathirika sana ni wanawake. Kwa mantiki hiyo, tulichunguza ubaguzi wa rangi na ubaguzi wa kijinsia.

Hatukujiingiza katika mtindo pamoja na kutambua kuwa Said A. Mohammed alitumia ujuzi mwingi kuiwasilisha riwaya hii kwani malengo yetu ya kimsingi yalijikita kwenye maudhui ya ubaguzi.

## 1.7 **MSINGI WA KINADHARIA**

Katika utafiti huu, tunaongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu/Uhalisiamazingaombwe kwani itaafiki utafiti wetu.

Wamitila (2003:234) anaeleza kuwa, Uhalisiajabu ni dhana iliyobuniwa na msanii wa Ujerumani, Franz Roh katika kitabu chake *Nach-expressionismus, magischer Realismus* na inahusishwa na waandishi wa Marekani ya Kusini au hata nchi zinazoitwa Ulimwengu wa Tatu na hutambulishwa na sifa mbalimbali. Sifa hizi ni za kuyaelezea matukio ya kifantasia au ya kiajabu au kichawi kwa namna ya moja kwa moja na kwa namna inayoyafanya yaonekane kama ya kawaida tu. Anasema kuwa, mpaka uliopo kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana huwa mdogo sana. Kulingana na Franz Roh, Uhalisiajabu ni uwasilishi wa ujumbe na hufichua hali ya kiroho na umazingaombwe katika jambo kwa kubainisha kudhihirika kwake na kuifanya zaidi ya kuwa halisi. Katika hali hii, Uhalisiajabu hutuingiza katika ulimwengu wa kinjozi kwa kuwasilishwa kama “uhalisi”.

Alexander, M. (1990:127), anaeleza kuwa, Uhalisiajabu ni kielelezo cha jinsi nadharia ya usasaleo inavyotuhimiza kuwaza upya juu ya dhana ya kimapokeo kuhusu riwaya ya Uhalisia ya karne za kumi na nane na kumi na tisa. Uhalisiajabu unatuhimiza kufikiria ufaafu wa baadhi ya mitindo tofauti ya uandishi kuangazia mada tofauti tofauti. Baadhi ya waandishi wanajadili uhusiano kati ya historia na masimulizi ya ubunifu, huku wakitumia visaasili katika kazi zao.

Kuna waandishi watangulizi wa uwanja huu wa uandishi miongoni mwao ni Topan katika tamthilia ya *Aliyeonja Pepo* (1970) na Hussein katika tamthilia ya *Mashetani* (1971). Watunzi

hawa wanakaribia kutumia mbinu Uhalisiajabu. Hata hivyo, ingawa waliweza kubuni hali za kiajabuajabu walifanya hivyo kwa kuchota mitindo yao kutoka malighafi ya utamaduni wa kiamerika na kiafrika ambapo tunajua tangu kale dhana za miungu, mashetani, pepo na nyinginezo zimekuwepo (Nyabunga: 2005).

Zamora na Faris (1995:4-5) wanasema: Uhalisiajabu ni mtindo wa kuandika na kuvuka mipaka, iwe ya kilugha, kisiasa, kijiografia au kibayolojia. Uhalisiajabu huwezesha kuingiliana na kuwepo kwa mandhari tofauti na hali kinzani ambazo kwa kawaida haziwezekani katika mitindo mingine ya uandishi.

Kimani na Chimerah (1999:200-201) wanatujulisha kwamba Juma na Kitaru wameamua kucheza mchezo wa shetani na binadamu ili waielewe barabara hali yao ya sasa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa jumla. Katika mchezo huu, kuna mgogoro uliopo baina ya shetani (Juma) na binadamu (Kitaru). Kitaru anafahamikiwa na migogoro, migongano na mikinzano ya kijamii katika ndoto. Kwa njia ya ndoto, anaifahamu mifumo mbalimbali ya kiuchumi na kijamii na jinsi inavyomwathiri yeye na jamii nzima. Kutokana na mchezo huu, tunaona jinsi ndoto kama mhimili wa uhalisiajabu inavyotumika kufunulia binadamu mambo anayokumbana nayo. Katika *Mhanga Nafsi Yangu*, ndoto kama mhimili wa Uhalisiajabu imetumika sana hasa kwa mhusika Afida ili kufichua hali yake ya kiroho na matumaini ya maisha mazuri Peponi.

Mbatiah (2001:93-94:) anasema: “Istilahi hii inatumiwa kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo na matukio ya kifantasia husawiriwa kwa kuiga mtindo wa uhalisia, yaani kwa kuyaeleza kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida.

Wasanii wanaoutumia mtindo huu hudhamiria kuonyesha kuwa ingawa mambo yanayoshughulikiwa ni ya kiajabuajabu, hutokea katika maisha ya kawaida ya jamii inayohusika.”

Gromov (2002:3-4) anaelezea kuwa, usasaleo ni njia ya kuufinyanga ukweli wa maisha kwa njia tofauti na jinsi ilivyozowewa.

Kulingana naye, Uhalisiajabu ni kitengo cha usasaleo ambacho kimefanikiwa kuzungumzia maswala ya kileo. Kutokana na maelezo haya, tunaonelea kuwa wasanii hawautumii Uhalisiajabu kiajali, bali kwa lengo la kuangazia hali ya jamii wanamoishi. Riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ni ya kimajaribio kwani nadharia ya Uhalisiajabu imetumika ambapo matukio halisi yanayotendeka katika jamii yanawasilishwa kwa njia mpya. Tasnifu hii itakuwa mojawapo ya kazi za kwanza kabisa kushughulikia ubaguzi katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* kwa kutumia nadharia ya uhalisiajabu.

Wamitila (2003:274) katika kutoa mchango wake kuhusu uhalisiajabu, anakubaliana na maelezo ya Mbatiah. Anasema: "Dhana hii huhusishwa na waandishi wa Marekani ya Kusini au hata nchi zinazoitwa Ulimwengu wa Tatu. Sifa yake kuu ni kuyaelezea matukio ya kifantasia au ya kiajabu au ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna inayofanya yaonekane kama ya kawaida tu." Mpaka uliopo kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana huwa mdogo sana. Sababu hasa ya matumizi ya mtindo huu ni kuonyesha kuwa matukio ya aina hii hupatikana katika maisha ya kawaida katika jamii zinazohusika, zinazoendelea kutoka bara la Afrika na Marekani ya Kusini.

Njogu na Wafula (2007:114) wanasema kuwa, Uhalisiamazingaombwe / Uhalisiajabu ni nadharia ambayo inakiuka sifa za uhalisia kama zilivyozoelewa na waandishi wa karne ya kumi na tisa na ishirini. Katika uhalisiajabu, matukio yasiyoaminika (ya kifantasia) husawiriwa. Mambo ya kiajabu yanaelezwa kwa namna ya moja kwa moja na kuonekana kuwa ya kawaida. Hali ya kushangaza na kuogofya huwasilishwa kuwa ya kawaida katika uhalisiajabu; ndoto na uhalisi vinachanganywa.

Huu ni ukweli unaobainika katika riwaya tunayoishughulikia ya *Mhanga Nafsi Yangu* ambapo msomaji yeyote wa hadithi hii anahisi kwamba, mambo yanayoelezwa kutokana na usawiri wa wahusika, mandhari, pamoja na usimulizi ni kama yasiyo ya kawaida lakini kwa hali halisi ni mambo yaliyowahi kutendeka katika jamii ila tu yanawasilishwa kwa mtindo mpya

D'Haen (2005:191) anaeleza kwamba, Uhalisiamazingaombwe ni tawi mahsusi la usasa baadaye (postmodernism), linaloonyesha sifa za usasa baadaye kama vile kujirejearejea, uziada uliopindukia uanuwai, mseto wa vitu, mwingilianomatini, kuchezea na kuyumbisha uthabiti wa wahusika na usimulizi vilevile kumchanganya msomaji kwa makusudi na hali kadhalika kufuta mipaka kati ya dhana, vitu au hali tofauti.

Kuhusu riwaya ya kimajaribio, Olali (2010:82-98) anathibitisha kuwa, riwaya kadha za Kiswahili zilizoandikwa tangu miaka ya 1990 hadi leo zinadhihirisha muundo usio wa kawaida zikilinganishwa na muundo wa riwaya ya kihalisia. Anaonyesha kuwa, katika riwaya za Kiswahili kuna ukiushi wa kisarufi ambao husababisha tofauti katika utaratibu uliozoeleka hadi kwa ule usiozoeleka. Olali (2010:83) anaonyesha muundo katika *Babu Alipofufuka* ambao ni mtindo katika riwaya za kimajaribio unaoingiliana na mambo ya kifantasia, kiajabu na wenye mitindo mipya ya uandishi wa kimajaribio ambao unajaliza katika masuala nyeti ya kimaudhui kama ya utandawazi, dini, filosofia na siasa za kimataifa.

Msisitizo wake wa sifa za riwaya hizi ni uandishi unaokiuka kaida za kiitikadi, utathmini wa ujumi kwa ndani na uvunjaji kaida za lugha kwa namna inayompa mwandishi uhuru zaidi. Anakiri kuwa msuko wa riwaya hizi ni changamano na hudhihirisha mbinu rejeshi kwa kiwango kikubwa. Kazi hii ina uhusiano mkubwa na kazi tuliyoiangazia kwani maudhui kwa jumla yanaangaziwa kutumia nadharia ya Uhalisiajabu ilhali kazi yetu imejikita kwenye maudhui ya ubaguzi. Kulingana na Olali (2010:83), msuko wa riwaya ya *Babu Alipofufuka* upo katika vitengo viwili, yaani wa mhusika mkuu K na wa mzuka wa babu yake. Pindi mzuka wa babu yake uanzapo kufuata maisha ya K, mambo ya kiajabu yanaanza kutendeka kama vile kupotea kwa chakula cha mbwa wake 'Doggy', kuendesha na aidha kusumbuliwa na mzuka uliomtawala mara kwa mara. Licha ya hayo, mizuka ya watu ambao alitendea mabaya hapo awali ilimrudiarudia, hawa walikuwa watu halisi ambao yeye pekee ndiye aliyewaona. Katika *Mhanga Nafsi Yangu*, kizuu cha baba yake Afida ambaye pia ndiye mhusika mkuu pia kinamtokea na kuzungumza naye, kwa hivyo kazi hii ina ulinganifu mkubwa kinadharia na kazi tuliyoiangazia.

Kutokana na fasihi simulizi za jamii za Wakikuyu (na zinginezo) mizimu huwatokea waliohai hasa ndotoni ili kujaribu kuelekeza jamii inapokosa mwelekeo.

Walibora (2010:143) akimnukuu Abrams ( 1999) anasema;
Istilahi ya 'Uhalisiamazingaombwe' ambayo mwanzoni ilitumika kuwahusu wachoraji katika miaka ya 1920, inatumika kufasili kazi za bunilizi za kinathari za Jorge Luis Borges wa Argentina, na hali kadhalika kazi za waandishi kama vile Gabriel Garcia Marquez wa
Kolombia, Isabel Allende wa Chile, Gunter Grass wa Ujerumani, Italo Calvino wa Italia, na John Fowles wa Uingereza. Waandishi hawa wanasukanisha uhalisia uliochongwa kwa njia maalum katika ruwaza inayobadilikabadilika daima, huku wakiwakilisha matukio ya kawaida na maelezo ya kina sambamba na vipengele vya kifantasia na kindoto, na kwa kutumia mambo yaliyotokana na visasili na hekaya. Riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* pia inazungumzia ukweli uliowasilishwa kwa njia ya kifantasia na kindoto licha ya kuwa mambo haya hutokea katika maisha ya kawaida.

Wasanii wanaotumia mtindo huu hudhamiria kuonyesha kuwa, ingawa mambo yanayoshughulikiwa ni ya kiajabuajabu, hutokana na maisha ya kawaida ya jamii inayohusika.
Kutokana na maelezo ya waandishi hawa, tunaona ya kuwa, wanauhalisiajabu hutumia sifa zinazobainisha kazi zao ingawa wana mitazamo na imani tofauti za kimsingi.
Huu ni ukweli unaobainika katika riwaya tunayoishughulikia ya *Mhanga Nafsi Yangu*
ambapo msomaji yeyote wa hadithi hii anahisi kwamba, mambo yanayoelezwa kutokana na usawiri wa wahusika, mandhari, pamoja na usimulizi ni kama yasiyo ya kawaida lakini kwa hali halisi ni mambo yaliyowahi kutendeka katika jamii ila tu yanawasilishwa kwa mtindo mpya.

Walibora (2010:146) anasema kuwa, Uhalisiamazingaombwe unapaswa kueleweka, kwa kadiri fulani, kama mkabala wa kuwakilisha uhalisia kwa kukiuka mipaka , kuhujumu au kuvuruga usimulizi mbali na kukaidi kaida za lugha na ingawa ni mkabala wa kifasihi unaonasibishwa zaidi na waandishi wa Amerika Kusini, umepenya kwingi duniani huku fasihi za janibu mbalimbali zikizungumzwa kwa dayalojia hii. Waandishi katika Afrika Mashariki waliotumia Uhalisia katika kazi zao za awali kama vile Ngugi wa Thiong'o mwishowe wameishia

kusombwa na wimbi hili la Uhalisiamazingaombwe hasa katika riwaya yake ndefu ya '*Wizard of the Crow*' (2005). Katika riwaya yake ya Kikuyu: *Murogi wa Kagogo* (2004:212), tunapata Uhalisiajabu ambapo mhusika mmoja anapoongea, sauti yake inasikika ikitoka ndani ya kioo. Vivyo hivyo, baadhi ya waandishi wa lugha ya Kiswahili kama vile; Said Ahmed Mohamed, E. Kezilahabi, K.W. Wamitila na Tom Olali wametekwa na 'mvuto wa ajabu' wa Uhalisiamazingaombwe. Wamitila (2003), katika '*Influence or Intertextuality?* A *comparative study of Kezilahabi's Nagona* and *Mzingile a*nd Juan Rulfo's *Pedro Paramo*; anabainisha jinsi fasihi ya Kiswahili inavyotoa mwangwi wa fasihi ya Amerika Kusini kwa kufumbata sifa za Uhalisiamazingaombwe. Yamkini makala za Wamitila za miaka ya 1991 (*Nagona* and *Mzingile*: Kezilahabi's metaphysics) na 1999 (Unlocking Katana Mkangi's Walenisi) ni miongoni mwa makala za kwanza kabisa kugusia uhusiano huu wa kimtindo kati ya fasihi ya Afrika Mashariki ya tapo hili na kwingineko.

Marquez kama mwasisi wa uandishi wa kisasaleo anafikiriwa na wasomaji wengi wa kimagharibi kuwa mwandishi wa kifantasia. Kinyume na madai haya, yeye mwenyewe amedai mara nyingi kuwa ni mhalisia ambaye anajaribu kuelezea jinsi hali ilivyo nchini mwake Kolombia kwa njia ya kweli iwezekanavyo. Williams anasema kuwa, Marquez (1980) anaelezea kuhusu wafanyakazi wa Macondo ambao wanaandaa mgomo. Baadaye uvumi unaenezwa kwamba serikali imewaua mamia ya wafanyakazi. Kisa hiki kimetajwa kuwa cha kifantasia kuliko vingine Kwa sababu tukio la kihistoria linapuuzwa na kuwasilishwa kama uvumi tu. Williams (1995:3). Nchini Chile, Allende (1985) ndiye mwandishi aliyeandika kazi zake za kwanza kwa kutumia mtindo wa Uhalisiajabu kuandika riwaya ya *The House of the Spirits*, inayohusu familia inayopitia mabadiliko ya kisiasa. Kama mtangulizi wake, anatumia Uhalisiajabu kuyaangazia masuala ya nchi yake yakiwemo siasa. (Encarta Encyclopaedia: 2002).

Wamitila anaendelea kuelezea kuwa, kazi ambazo zinaweza kuelezwa kama za kihalisiajabu huchanganya sifa za kihalisia na kiajabu au maajabu. Anatoa mifano ya wahusika wanaopatikana kwenye riwaya ya Marquez, *One Hundred Years of Solitude* ambao wanaishi chumba na choo

bila kutambua na pia kupaa angani na shuka ya jirani. Anasema kuwa, wahusika wengi wa Juan Rulfo katika *Pedro Paramo* ni wafu na msimulizi wa hadithi anaendelea kusimulia hata baada ya kufariki. Katika riwaya ya *The House of the Spirit*s ya Allende, kuna msichana (Rosa) anayezaliwa akiwa na nywele za kijani na rangi ya uso wa manjano (Wamitila 2002:118).

Waandishi wa kazi hizi wanayakiuka matarajio ya uhalisia wa kisimulizi kimakusudi. Mpaka uliopo kati ya yanayowezekana (mambo halisi) na yasiyowezekana unafutwa. Kazi hizi zinavunja muundo wa kikawaida wa utanzu kama njia ya kuzuka na istiara ya miundo ya mifumo ya kisiasa, kiuchumi na kitamaduni ya ulimwengu (Wamitila 2002:117).
Kutokana na kazi za Danow (1995), Zamora (1995), Cooper (1998), Mbatiah (2002) na Wamitila (2003), tunapata kuona kuwa, uhalisiajabu ni namna fulani ya kueleza uhalisi unaotuzunguka kwa njia mpya.

Katika utafiti wetu, tulitumia kanuni zifuatazo za nadharia hii ya Uhalisiajabu;

i. Kueleza matukio ya kiajabu au ya kifantasia au ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja na kuyafanya yaonekane ya kawaida. Huwepo hali ya kushangaza, kuduwaza na kuogofya. Katika Mhanga Nafsi Yangu, kizuu cha babake Afida kinatokea na kuzungumza naye kana kwamba ni jambo la kawaida tu ilhali katika uhalisia katika jamii, jambo hili ni la kuogofya na kushangaza.

ii. Uhalisia na ndoto vinachanganyika. Huwa hakuna mipaka ya uhalisi na utohalisi katika uhalisiajabu. Pengine wakati mtu anapoota ndipo yupo uhalisini na wakati yupo uhalisini ndipo yumo ndotoni. Uhalisia wa maisha ya Afida ni kwamba yana matatizo yanayotokana na dhuluma na ubaguzi wa Wapeponi, hata hivyo, kila anapoanza kuuona uhalisia huu, huwa anaota na hujuta zaidi na kuogopa hali yake ilivyo akiwa ndotoni.

iii. Mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa huvunjwa. Yaani, wana-uhalisiajabu wanajadili mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla bila ya kujiweka katika mazingira finyu kama vile ya

jamii, nchi au bara fulani. Riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* imezungumzia maswala yanayotokea katika mabara mawili. Hii ni wazi kuwa mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa imevunjwa.

iv. Wakati na mwanda (mahali/mandhari) hupanuliwa na kuwa na uhusiano mkubwa. Mpaka wa jadi baina ya nyakati huvunjwa kiasi kwamba matukio hayafuati kanuni ya uhalisi wa kiwakati. Mara nyingi mtazamo huu wa wakati unafungamana na suala la ndoto. Katika hali hii, mtunzi huweza kueleza kile kinachomkumba binadamu kabla ya kuzaliwa na baada ya kifo. Ukweli wa kauli hii katika *Mhanga Nafsi Yangu* ni kuwa tunaelezwa maisha ya babake Afida baada ya kifo chake. Mwanda wa kisimulizi pia hupanuliwa. Huweza kuhusisha ulimwengu halisi, ulimwengu wa kidhanifu au ulimwengu wa kinjozi na maingiliano kati ya aina hizo tofauti huvunjwa. Hali hii humwezesha msimulizi au mhusika kujitosa kwenye tathmini ya kisaikolojia. Katika *Mhanga Nafsi Yangu* Afida amechorwa kama mhusika mwenye nafsi mbili. Kuna nafsi moja ya Afida ambayo inaishi katika ulimwengu halisi na nyingine katika ulimwengu wa kinjozi.

v. Matukio hayafuatani kimantiki kama ilivyo kawaida. Huwepo mvunjiko katika usimulizi. Wasanii huweza kutumia mbinu ya ukumbukaji, mbinu rejeshi, mtiririko wa urazini na ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili. Katika *Mhanga Nafsi Yangu*, mbinu hizi zimetumika hasa Afida anapokumbuka mawaidha ya babake kabla hajafa, mbinu rejeshi pia imetumika kwa matukio mengi mojawapo ikiwa ni kuelezwa kwanza Afida akiwa safarini na kufika Uropa na tunarejeshwa katika maagano ya Afida na ukoo wake. Afida amejengwa kama mhusika mwenye nafsi mbili.

vi. Mazingira huwa ni sehemu muhimu katika aina hii ya fasihi. Wanyama, majitu/ mazimwi na misitu mikubwa yenye giza totoro hurejelewa. Pia, mimea, mito, maziwa na bahari huchukua nafasi muhimu katika uandishi wa uhalisiajabu. Tunakumbana na hali ya kuogofya katika mazingira kinakotokea kizuu cha baba Afida. Mitetemeko, mwangaza na pia kizuu chenyewe kinaduwaza.

vii. Uhalisiajabu unahusisha kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu. Hali mbalimbali kama uhalisi na ndoto, kifo na uhai, usasa na uzamani, shamba na mjini, ugeni na

wenyeji/utamaduni huonekana zikiingiliana. Kadhia hizi zote ni uhalisia wanaokumbana nao wahusika katika *Mhanga Nafsi Yangu*. Uhalisi na ndoto zinaingilliana katika maisha ya Afida, kifo na uhai ni hali ambazo hazina mipaka halisi tukiangazia maisha ya babake Afida, shamba na mjini ni hali zinazoingiliana kwani maisha ya Afida na Shuhuda yanaelezwa wakiwa katika hali hizi mbili. Ugeni na wenyeji  pia ni maswala yanayoonekana kupitia Waafrika waliohamia Peponi na kuwa wenyeji wakiwemo Bi Marneti na Prof. Marjan.

Katika nadharia ya uhalisiajabu, ndoto *huchukua* nafasi muhimu sana kwani matukio mengi hutokea wakati mtu anapolala au yumo mawazoni. Malcolm, N. (1959:94) anaeleza kuwa, ndoto ni mtiririko wa mawazo ya ndani ya mtu aliye macho au anayelala yanayoambatana na maono, taswira za matukio, mazingaombwe, fikira za uwongo, udhanifu, ndoto za mchana, ukisiaji, uwepo na malengo, matarajio na matamanio. Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa ndoto huambatana na picha na mawazo na matukio kama kwamba yanatokea katika hali halisi.

**1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA.**

Kwa mujibu wa Beauvoir (1949), utiifu hauhusishwi miongoni mwa majukumu ya mwanamke. Alidai kuwa, kila mwanamke nchini Ufaransa ana uhuru wa kujiamulia mambo lakini nyanjani uhuru huo haupo. Ni uhuru kidhahania kwa sababu hauambatani na uhuru wa kiuchumi. Mwanamke anayemtegemea mumewe hawezi kuwa na uhuru wa kujiamulia mambo kwa sababu mila na desturi hazimruhusu na zinatumika kumbagua. Hali kama hii ni yakini katika baadhi ya mataifa na jamii hususan bara la Afrika. Uhuru ambao ni hasi haujaleta mabadiliko kwa mwanamke. Amekubaliana na hali yake ya kuwa mwanamke huku akiishi kwa kuvumilia matatizo mengi. Ni kupitia kwa ajira ambapo mwanamke ataweza kujinasua kutokana na hali ya unyanyasaji unaotokana na mila. Hakuna njia nyingine mwafaka ambayo inaweza kumhakikishia uhuru wake maishani isipokuwa hiyo ya ajira. Pindi tu atakapoacha kuwa mtegemezi na kujitosheleza katika baadhi ya mahitaji, mfumo wa kutegemewa utabadilika na hatakumbana na madhila mengi yanayohitaji kuangaziwa au mtu wa kutegemea kuleta suluhu la masaibu

yanayomkumba duniani. Kule kumtegemea mwanamume ndiko huyu mwanaharakati anadai kuwa ni chanzo cha unyanyasaji na ubaguzi. Jamii haijaweka mikakati ya kutosha ili kuleta mabadiliko kuhusu hali ya wanawake ya kubaguliwa.

De Beauvior, (1952), katika kitabu cha, *The Second Sex,* anaonyesha ubaguzi wa mwanamke na jinsi alivyodunishwa katika asasi ya ndoa, dini na utamaduni ambapo huchukuliwa kama msaidizi wa mwanamume na kwamba mwanamume ndiye anayepaswa kuchagua mpenziwe. Anaendelea kusema kuwa ndoa imejengwa kwenye misingi na imani ya uwezo mkubwa alionao mwanamume akilinganishwa na mwanamke Kazi hii ya Beauvoir ni muhimu kwetu kwa sababu ametaja unyanyasaji na ubaguzi unaotokana na mfumo wa kijamii. Unyanyasaji ni kipengele miongoni mwa vipengele tulivyovichunguza kama changamoto zinazosababishwa na baadhi ya wanajamii hususan wanaume. Bado ulimwengu huu una baadhi ya sehemu ambazo zimethibitiwa na mifumo ya kijamii ambayo huwakweza wanaume na kuwatweza wanawake. Ni wanawake wachache tu ambao wana imani inayofungamana na misingi ya kisiasa ambao wamechukua hatua ya kujinasua kutoka kwa tatizo hili la ubaguzi. Kazi hii ni muhimu kwetu maana itatusaidia kulinganisha na kuchunguza mwanamke wa Kiafrika anavyobaguliwa Peponi katika *Mhanga Nafsi Yangu*.

Kulingana na Woolf kama alivyonukuliwa na Coser (1963), "mwanamke hawezi kupata ukombozi wa aina yoyote kama hajakombolewa kiuchumi. Kwa ujumla katika jamii nyingi ulimwenguni, nyenzo zote za kuzalisha mali zinatawaliwa na wanaume huku wanawake wakibaguliwa na kuwa wategemezi na watumishi wa wanaume. Hali hii huwakumba wanawake kwa sababu tangu zamani wanawake wamenyimwa nafasi ya kujiendeleza kiuchumi". Woolf kama alivyonukuliwa na Coser anapendekeza kuwa; mwanamke apewe uhuru wa kiuchumi ili aepuke ubaguzi, unyanyaswaji na dhuluma. Iwapo jamii itakubaliana na wazo hili la Woolf, ni bayana kuwa unyanyasaji na dhuluma kwa mwanamke utapunguzwa kwa kiwango fulani. Vile vile jamii nyingi za kisasa zimehamasishwa na zimeaanza kuwa na mtazamo chanya wa kuwapatia wanawake fursa ya kujiendeleza kiuchumi kupitia uundaji wa vikundi vya wanawake kama itakavyobainika kwenye uchunguzi wetu.

Berkely, katika kitabu chake *The Anatomy of Racial Attitudes* (1983) anaeleza jinsi ubaguzi unavyoendelezwa kisiasa, kirangi na vile jinsia ya kike inavyobaguliwa. Kitabu hiki kina manufaa sana kwani kazi yetu imesheheni ubaguzi wa rangi na wa jinsia. Afida ambaye ni wa jinsia ya kike anabaguliwa na kudhulumiwa pamoja na wenzake wanawake na kuishia ulevini na ukahabani.

Mukobwa (1985) ameshughulikia *'Maendeleo ya kimaudhui katika tamthilia za Ebrahim Hussein'.* Amezungumzia kipengele cha maudhui ambacho vile vile nasi tutashughulikia huku tukiangazia ubaguzi. Alitumia nadharia ya ki-Marx kujikita katika uhalisi wa kihistoria, utafiti wetu utajikita katika nadharia ya Uhalisiajabu ili kutuongoza kuangazia ubaguzi. Tunakubaliana na ufafanuzi wake kuhusu ubaguzi wa mwanamke ila yeye amekusanya data ya utafiti wake kutoka tamthilia za Hussein, na sisi tutakusanya data ya utafiti wetu kutoka riwaya ya Said. A. Mohammed.

Gordon D. (1986), katika kazi yake ya *Apartheid; (Tragedy in black and white),* anaeleza ubaguzi wa rangi na jinsi unavyoendelezwa kwa kunukuu vibaya vitabu vya dini, pia anaeleza jinsi watu wengi wanavyotafsiri kitabu cha Biblia vibaya ili kuendeleza ubaguzi. Kazi hii itatusaidia sana katika utafiti kwani tutazingatia baadhi ya maswala hayo. Ubaguzi wa rangi katika *Mhanga Nafsi Yangu* unaonekana, na asasi mbalimbali zinatumika kuuendeleza ubaguzi huu hasa elimu na dini.

Chesaina (1987) alitumia tamthilia ya Mlama (1972) *'Hatia'* na tamthilia ya Muhando (1982) '*Nguzo mama'* na kueleza ubaguzi unaomkabili mwanamke katika hali zake zote za maisha. Tofauti na yeye ni kwamba sisi tutatumia *Mhanga Nafsi Yangu* ambapo tunaangazia ubaguzi kwa wanawake na wanaume na kazi yake itatusaidia kuangazia masaibu yanayomkumba mwanamke hasa kwa kuyachunguza aliyoandika kuhusu *Nguzo mama*. Bila shaka utata anaouzungumzia ndio utakuwa kwetu darubini ya kuangazia ubaguzi katika kazi yetu.

Lugano (1989) aliandika na kuonyesha picha ya ubaguzi wa mwanamke katika siasa na mambo ya kijamii kwa kumulika riwaya za Kezilahabi. Alionyesha kuwa mwanamke anachorwa kama kiumbe anayetegemea mwanaume. Kauli hii ni muhimu kwetu kwa sababu itatusaidia kuchunguza na kubainisha uhalisia wake na athari zinazoibuka kutokana na ubaguzi. Mirengo ya nadharia zote za kijamii humulika mifumo ya jamii na katika mfumo wowote ule, kipengele cha utegemezi hakiwezi kukosekana. Kipengele hiki kitatusaidia kuchunguza ubaguzi na unyanyasaji wa kijinsia.

Sigelman Lee na Susan Welch (1994) katika kitabu chao *Black Americans View of Racial Inequality* pia wameeleza maoni ya Wamarekani weusi kuhusu chanzo cha ubaguzi wa rangi kutokana na wenzao weupe. Kazi hii itatufaa sana katika utafiti wetu kwani ni dhahiri kuwa ubaguzi anaozungumzia pakubwa Said A .Mohamed katika *Mhanga Nafsi Yangu* ni wa kirangi.

Mwita (2005) anasema kuwa, kutokana na mfumo wa kuumeni uliokithiri katika jamii ya Wakuria, hali halisi ya mwanamke inaonekana iliyojaa ubaguzi, dhuluma, unyanyasaji na unyonyaji. Mwanamke daima anabaguliwa. Hali zote za maisha yake hutegemea uamuzi wa mwanamume. Kujiamulia mambo kwa wanawake katika jamii hiyo ni sifa hasi. Anatamatisha kwa kusema kuwa hali hii ni yakini katika jamii nyingi za Kiafrika.

Sisi tunakubaliana naye ila kipindi tulicho nacho kwa sasa hali imebadilika. Kipindi cha miaka ya nyuma hali ilikuwa jinsi Mwita anavyoeleza. Mabadiliko tunayoyashuhudia sasa yameletwa na maendeleo ya elimu ya mtoto msichana na uhamasishaji unaoendelezwa na wanaharakati wakisaidiana na baadhi ya wafuasi wa madhehebu ya kikristo. Pia mashirika yasiyo ya kiserikali yametoa na yanaendelea kutoa mchango kuhusu uhamasishaji wa umma juu ya maswala yanayowahusu ubaguzi wa kijinsia. Kazi hii ni muhimu kwetu kwa sababu itatusaidia katika uchambuzi na ufafanuzi wa swala la ubaguzi katika *Mhanga Nafsi Yangu.* Kazi yake ni tofauti na yetu kwa kuwa uchunguzi wake ni kuhusu *"dhima ya ichingero za Wakuria katika kusawiri ubaguzi kwa mwanamke".*na uchunguzi wetu ni kuhusu "*ubaguzi katika Mhanga Nafsi Yangu*".Uchunguzi wake ulikuwa wa nyanjani na wetu umetumia matini za riwaya.

Katola (2006) ameshughulikia "Ubaguzi na Udhalimu Dhidi ya Wahusika wa Kike katika Tamthilia Nne za Kiswahili." Tamthilia hizo ni za waandishi wa jinsia tofauti ambao ni Muhando, *Hatia* (1972), Mwachofi *Mama Ee* (1987). Hawa ni waandishi wa kike. Waandishi wa kiume ni Yahya na Mulwa, *Buriani* (1983) na Mohamed *Kitumbua Kimeingia Mchanga,* (2000). Katika kazi yake hakuegemea upande wowote wa waandishi ila ameonyesha kuwa mwanamke anadhulumiwa na mifumo ya kiume katika taasisi ambazo zimejikita kwenye misingi ya ubabe-dume. Baadhi ya dhuluma alizotambua ni wanawake kutishwa, kutusiwa, kuozwa bila hiari, kupigwa, kunyimwa haki na kukataliwa na jamii miongoni mwa zingine. Matokeo yake ni mtazamo hasi kwa mwanamke katika jamii. Katola ametumia nadharia ya ufeministi wa Kiafrika. Kazi hii imekuwa ya manufaa kwetu kwa sababu mtazamo wake kuhusu dhuluma na ubaguzi wa kijinsia umetupatia mwanga kutambua zile dhuluma kama ambazo anakumbana nazo mwanamke na zinaweza kutafutiwa suluhu mwafaka na kupunguzwa iwapo haziwezi kukomeshwa kabisa. Mirikau, S A (2011), akimnukuu Mule K. (1991) anazungumzia ubaguzi kati ya wanawake kwa wanawake wenzao. Anawapa motisha wanawake kujiendeleza na kuwapenda wenzao ili kujiendeleza. Hii ina umuhimu katika kazi yetu kwani inadhihirika wazi kwa sababu adui mkubwa anayeanzisha mateso dhidi ya mwanamke Afida ni mwanamke. Wanawake wengi katika riwaya tunayoishughulikia hawapendani na hii inasababisha madhara mengi kwa maisha yao.

Matundura Enock (2007) katika tasnifu yake kuhusu "*Taswira dumifu za uana katika fasihi ya Kiswahili ya watoto,*" anasema kuwa mkabala wa kiuana unajishughulisha na maswala ya kimahusiano katika jamii. Mahusiano yanajibainisha katika misingi mbalimbali kama vile kijinsia, kitamaduni, kiutendi kazi, kiu-asasi. Pia ametumia mkabala wa nadharia ya ufeministi ambao ni mkusanyiko wa 'nadharia' nyingi ambao kimsingi lengo lake ni kuleta usawa kati ya wanawake na wanaume. Kazi hii imekuwa ya manufaa kwetu kwa sababu tumepata mambo muhimu ambayo tunafikiri yatajitokeza katika kazi yetu ili kuangazia ubaguzi wa kijinsia.Hata hivyo kazi yake ni tofauti na yetu kwa sababu amechunguza taswira dumifu za uana katika

*Msichana mlemavu na ndugu zake, Mwanasesere wa Mosi* na *Mgomba changaraweni*. Pia ameangazia taswira dumifu katika *Ndoto ya Riziki, Siku ya wajinga* na *Alitoroka*

Maingi H. (2011) amefafanua ubaguzi wa jinsia ya kike katika asasi za kijamii kama vile dini, ndoa na elimu. Ameonyesha kuwa dini ni mhimili mkubwa katika imani na itikadi za jamii na huupa nguvu ubabedume ambao nao hupelekea kukandamizwa kwa mwanamke kielimu na katika ndoa. Amenukuu Korani Takatifu sura ya 24:32 inavyowahimiza wanawake kuinamisha nyuso zao, na kutodhihirisha mapambo yao, watubie kwa Mwenyezi Mungu ili wapate kufaulu. Mtume Paulo katika dini ya Kikristo naye aliwahimiza wanawake kuwatumikia waume zao. Huu ni upembezwaji wa jinsia ya kike ambao unapelekea ubaguzi wa kijinsia. Wahusika wa kike katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* pia wamebaguliwa. Ubaguzi wa kielimu na dhuluma ya wanawake katika ndoa hasa kwa mhusika Afida anayenyang'anywa mtoto, jambo lililopelekea kifo chake.

Kitali (2011) ameshughulikia fani na usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia ya *Pango* na *Mama Ee*. Kuhusu tamthilia ya *Pango,* anasema kuwa, tatizo kuu linahusu siasa, uchumi, uongozi na migongano ya wimbi la ukale na usasa. Kuhusu tamthilia ya *Mama ee,* anasema ni mchezo unaoyasawiri matatizo yanayoikumba ndoa ya Mwavita na mumewe Kinaya. Pia ameangazia mahusiano ya wanawake na wanaume katika jamii, nafasi ya mwanamke katika jamii, taasubi ya kiume na ubabedume ambao umejikita katika jamii. Sisi tutashughulikia aina zote za ubaguzi ukiwepo wa kijinsia.

Mwelekeo wetu utatusaidia kugundua ikiwa madai mengine nyeti kama vile 'haki' na 'usawa' yanakubalika kulingana na kaida za kijamii au ni kwa jinsi gani mfumo wa kisheria utasaidia kuinua kiwango cha utekelezwaji. Pia tutajaribu kuchunguza sehemu ambazo dhana ya 'usawa' haiwezi kuwa ni uhalisia. Dhana ya usawa kukosekana ni yakinifu kulingana na Honore de Balzac (1799-1850) jinsi alivyonukuliwa na Coser (1963) kuwa: *"Usawa ni 'haki' lakini hakuna mamlaka wala nguvu hapa duniani ambayo yanaweza/zinaweza kugeuza dhana hii kuwa ya kweli na halisi".* Hii inasisitiza dhana ya ubaguzi kama tunavyoushughulikia

## 1.9 MBINU ZA UTAFITI.

Utafiti wetu ulikuwa maktabani. Tulisoma riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ya Said A.Mohamed. Tulijikita katika uchanganuzi wa maudhui ya ubaguzi. Aidha, tulisoma vitabu, majarida na tasnifu za waandishi wengine ambazo zina uhusiano na ubaguzi. Tulisoma yaliyoandikwa kuhusiana na mwelekeo wa kihakiki wa uhalisiajabu katika vitabu na makala mbalimbali na pia mtandao. Maelezo haya yalituwezesha kuelewa nadharia hii kwa kuangazia jinsi misingi ya madai yake inavyotumiwa katika uhakiki wa mada yetu na kwa njia hiyo kufanikisha utafiti wetu.

Pia, tulitafuta ushauri kutoka kwa wasimamizi wetu, wahadhiri mbalimbali wakiwemo wanafasihi na wanaisimu. Tajriba yetu na pia ya jamii zetu kuhusu ubaguzi zilitoa mchango mkubwa katika kubainisha ubaguzi.

Tatu, tumesoma yaliyoandikwa kuhusu riwaya za kimajaribio (riwaya mpya), kuhusu ubaguzi na Uhalisiajabu katika riwaya za Kiswahili ili kujua pengo lililoachwa ambapo tulibaini kuwa, ubaguzi wa kijinsia tu ndio uliozungumziwa kwa tafiti nyingi lakini haukuhusishwa na wa kirangi kama tulivyofanya katika kazi yetu. Uchunguzi wetu umetuwezesha kuchangia mada yetu kwani riwaya hizi zimeonyesha upeo wa juu wa dhana za ubaguzi Uhalisiajabu.

Nne, tumesoma yaliyoandikwa kuhusiana na mwelekeo wa kihakiki wa Uhalisia mazingaombwe katika vitabu na makala mbalimbali na pia mtandao. Maelezo haya yametuwezesha kuelewa nadharia hii kwa kuangazia jinsi misingi ya madai yake inavyotumiwa katika uhakiki wa fasihi na kwa njia hiyo kufanikisha ufahamu wetu na utafiti wetu. Tajriba yetu na pia ya jamii zetu kuhusu ubaguzi zimetoa mchango mkubwa katika kuubainisha. Tumeweza kuwahoji baadhi ya waandishi wanaotumia Uhalisiajabu na kupata maoni yao kuhusu msukumo uliowafanya kutumia mwelekeo wa Uhalisiajabu**.**

# SURA YA PILI

## TATHMINI YA JAMII YA *MHANGA NAFSI YANGU*

### 2.1 Utangulizi

Jamii ya *Mhanga Nafsi Yangu* jamii ya Kiafrika iliyo katika mpito, ni jamii iliyosongwa na matatizo ya aina nyingi; kusambaratika kwa familia, kuhama kwa wanafamilia, ufukara na uhaba wa bidhaa na huduma na mbano wa fursa unaopelekea wanajamii hawa kuwa na hali ngumu ya maisha.

Sura hii inachunguza ubaguzi, tofauti za kitabaka, mikinzano ya maisha na hatua za binadamu katika maisha yake. Mohamed anawatumia wahusika wa kawaida wanaoiwakilisha jamii ya kisasa inayokumbwa na mabadiliko mengi yanayowasukuma kufanya vitendo tofautitofauti. Wahusika hao ni pamoja na Afida, Bi. Marneti, Shuhuda,

Neshboch, She-Shaiza, Yakrobich, Shaabani, Bi. Mwamda, Kisura na Profesa Marjan.Vilevile, mwandishi anaibua wahusika wa kihalisiajabu kama vile kizuu cha baba yake Afida na sauti ya ndani ya Afida. Matatizo wanayoyapitia wahusika yana vyanzo. Riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* inayaangazia masaibu yanayomkumba Afida anapotoka kwao Motoni na kuelekea ugenini Peponi kujitafutia riziki. Motoni inawakilisha mojawapo ya nchi barani Afrika inayokumbwa na matatizo ya umaskini, njaa, magonjwa na kubakia nyuma kimaendeleo. Nayo Peponi inawakilisha taifa nje ya Afrika lililo na ufanisi mkubwa katika nyanja za kijamii, kiuchumi, kielimu, kisheria na kiteknlojia.

Katika sehemu hii, tunaonyesha kwa kina jamii katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ilivyosawiriwa. Hii ni kwa sababu lazima tuielewe jamii kwanza ili tuyaweke bayana na kwa kina masuala muhimu tutakayokabiliana nayo pamoja na mawanda yake kwa kuyafafanua na

kuyatolea mifano. Aidha, litakuwa jambo la kufaa kuieleza dhahiri riwaya yenyewe ili data tutakayoishughulikia iwe ya kutusaidia katika kufanikisha malengo yetu ya utafiti.

Masuala haya ni ya kimsingi na kuyashughulikia vyema katika sehemu hii kutafaulisha na kurahisisha tunayotafiti na kuhimili msimamo wetu. Nadharia ya Uhalisiajabu itatusaidia pakubwa kwani mwandishi amevuka mipaka ya kitaifa na kilugha. Mazingira, matendo na matukio ya kifantasia yamesawiriwa kwa kuiga mtindo wa uhalisia, yaani kwa kuyaeleza kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida. Mfano ni pale Afida anapozungumza na babake aliyefariki na pia anapochorwa kama mhusika mwenye nafsi mbili. Mipaka ya kijiografia imevunjwa kwani riwaya hii imejikita katika bara mbili. Ndoto, kumbukizi na urejeshi pia zimetumika ili kusawiri matukio riwayani. Ingawa mambo yanayoshughulikiwa ni ya kiajabuajabu, yametokea katika maisha ya kawaida ya jamii inayohusika na ndiposa nadharia hii itafaa katika uhakiki wetu. Mpaka uliopo kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana ni mdogo sana kama tulivyoeleza katika sura ya kwanza.

## 2.2 Riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* kwa muhtasari.

Katika riwaya hii, tunachorewa dunia iliyoharibiwa na kufisidiwa. Hakuna kulikotulia duniani kumfanya mtu achote riziki yake. Mhusika Afida ni mfano bora wa mtu aliyejitolea mhanga kwa matarajio ambayo kuanzia mwanzo hayakuwa na msimamo. Afida anaikimbia nchi na watu wake kwenda kuishi na kutafuta riziki yake peponi. Anahajiri na kuishi peponi kwa sababu kwao hakuna maisha yoyote ya maana. Safari yake imejaa matumaini ya kupata elimu bora, maisha mazuri ya utajiri, mapenzi na furaha.

Mara tu Afida anapofika Peponi, matumaini yake yanagonga mwamba, Shangazi yake Bi. Marneti aliyemfanyia wema wa kumleta Peponi ndiye anayekuwa adui wake mkubwa. Kisha, mazingira ya Peponi na fikra mbaya walizonazo wenyeji kuhusu wageni hasa wageni weusi. Yanakuwa ni mazingira ya ubaguzi na udhalilishaji kwani maisha ya Afida yanakuwa magumu

kiasi kwamba hawezi kuyadhibiti tena. Matumaini ya Peponi yanageuka kuwa balaa. Kiapo cha mapenzi alichomwapia Shaaban (mpenziwe wa Motoni) kinasahauliwa. Ahadi alizoahidi ukoo wake atatimiza akifika Peponi zikavunjwa. Matumaini mema yakakatika na akakata tamaa. Hapo, usafi wa roho na maadili ya Afida yakachafuka na baadaye kapotea asijulikane alikokwenda.

Hadithi inaanza Afida akiwa ndani ya Air Uropa akielekea Peponi. Ana mawazo mengi sana ambayo yanamfunga kuitawaza furaha. Furaha anayopaswa kuwa nayo kwani amepata bahati njema ya kwenda Peponi. Kwenye mawazo ya Afida tunarudi nyuma katika mwagano na ukoo wake mkubwa katika uwanja wa ndege wa kimataifa. Afida anaeleza kuhusu mshikamano wa ukoo unavyozidi kuwaangamiza kwa kuwa Waafrika lazima wagawane mafanikio yote. Katika mwagano Afida anatoa ahadi kwa; Bi. Zaina, Bi.Sinangoa, Bi. Mwamda (mamake), Kisura na jamaa zake wote wanakuwa na matumaini naye. Vilevile akiwa ndani ya Air Uropa, anajisaili kuzaliwa mtoto wa kike, na kuhusu sababu ya wageni wengi kuondoka makwao kuja Motoni.Babake Afida Bwana Daudi, anajitokeza ndotoni ya Afida na hamwitikii wala hataki kumkumbatia Afida kama alivyofanya zamani alipoona babake yu tayari kuondoka kwa safari ya muda mrefu.Kwenye ndoto Afida anakumbuka mafunzo ya mwalimu wake,uhusiano wake na babake katika utoto wake. Baadaye Afida anagutuka kutoka kwenye ndoto, anapata ndege ikiwemo katika hatua ya kuteremka katika uwanja wa ndege wa Peponi,na anagundua kila kitu ni cheupe Peponi. Ukurasa mpya wa maisha ya Afida Peponi unaanza. Ni majira ya baridi Peponi na hawezi kulala kwani baridi ilipenya kila kipembe na kumwingia hadi mifupani kila siku.Yuko ndani ya kujichumba kidogo anamolala ambamo hamkuwa na vukuto la joto la kutosha, huku shangazi yake Bi. Marneti na mumewe Bwana Bawa wakiishi kwenye chumba kikubwa kilichojaa uvuguvugu na raha.Tunaona nyumbani kwa Bi. Marneti kumejaa samani na vifaa vya haja ya usaidizi wa binadamu. Afida anakumbuka mwalimu wake wa somo la siasa alivyowahi kuwaonya shuleni juu ya utashi wa vitu.Alisema utashi wa vitu ni haja na fahari ndiyo unaambatana na balaa. Afida aliona tu ni choyo ya kukosa kumiliki vifaa hivyo. Tunaangaziwa mwezi mmoja tu baada ya Afida kufika Peponi anapomsikia shangaziye Bi. Marneti na mumewe wakigombana.Bw.Bawa anasisitiza lazima alazwe kwenye chumba chenye joto la kutosha kwani si uungwana kumlaza kwenye chumba kile chenye baridi ya kumtia mtu maradhi, naye Bi.

Marneti anasisitiza alazwe huko azoee baridi na ndivyo ilivyo sasa. Asubuhi anaamka na kitetemeshi, cha mwili na mafua Bi. Marneti anampeleka hospitali na njiani anamwonya kutotazama kwa mfululizo macho ya Mwani kwani yana mvuto wa ajabu. Zahanatini Bi.Marneti anadanganya daktari kuwa Afida analala kwenye chumba chenye vuguvugu la kutosha.Baadaye Afida anatukumbusha kuwa anakatazwa na Bi. Marneti kukoga kila siku kwani Peponi hakuna joto kama Motoni, na hata akikoga mara milioni kutwa moja hatakuwa mweupe kama wapeponi. Siku hii Afida akinyatianyatia kwenda kukoga anasikia ugomvi baina ya Bi. Marneti na Bw.Bawa. Bwana Bawa alisema Bi.Marneti alimwonea wivu Afida ambaye ni mwanaye na mtoto wa dadake. Bi.Marneti anakana wivu na kueleza kuwa alitaka Afida apelekwe shule akasome.Wanadhihirisha kuwa maisha yao yameharibika tokea kuja kwa Afida. Baada ya kukoga Afida yuko chumbani mwake, hana kitu au mtu wa kusema naye na hivyo basi anaanza kusema na sauti.Alisema kuhusu kukerwa na masusuiko ya Bi. Marneti nayo sauti ilizungumza kuhusu wenye pesa ambao hununua vitu kwa mchezo tu, si kwa haja na wale wanaoweza kuhasiri roho za watu wasio na hatia kupata wanachotaka.Vitu hivi ndivyo vilivyobadilisha upya mawazo ya Afida.Afida anatuonyesha maisha ya Bi. Marneti yalivyokuwa akiwa Motoni alikuwa hana ugomvi, alipenda mapenzi safi na vilevile mwenye kuchangua maneno ikitofautishwa sasa alivyo mgomvi na mwenye kupenda watu walio mbali yaani Wapeponi. Tunapelekwa mbele siku ambayo Afida amesimama peke yake kwenye kituo cha basi. Ni majira ya baridi na amejifunika maguo mazito mazito mwili mzima.Amegundua mambo kuhusu Wapeponi; kila kitu kinaendeshwa kwga wakati, Jumapili si siku nzuri ya kutoka, kwani ndio siku wapeponi hupumzika na kujifungia ndani ya majumba yao. Yeye ametoka kwani amechoka kuketi ndani na kukerwa na nafsi yake, anataka kuzururazurura nje. Akingoja basi anamkumbuka mwalimu wake wa fasihi, Mzee Dawamu alivyowasaidia kuchambua shairi la majira ya baridi Peponi. Ingawa awali alikana shairi lile sasa anaona mawazo yake ni ya uhakika na kamilifu. Ndani ya basi anaketi na kuingia ndotoni, anakumbuka Motoni msimu wa kipupwe wakati kuna mboga na matunda ya kila aina. Ndipo maskini husimamisha vimeza na vigari vibovu kando mwa barabara kuuza matunda ili kukusanya faida chache za kulisha koo zao kubwa. Hawa pia ndio hupigwa picha sana na watalii. Miezi tisa inapita na watu wengi katika ukoo wa Afida wamemwandikia barua na kumuuliza hali na kumkumbusha wajibu wake. Amewajibu wachache

tu, tena kwa nadra,na hivyo wamekasirika na kusema kwenye barua kuwa yeye ni msaliti wa ukoo. Anapukutikwa na machozi akikumbuka ladha tamu ya mapenzi yake na Shaabani yanavyozidi kufifia. Zaidi ni kuwa watu wa ukoo wanaagizia vitu wakati yeye mpaka sasa hana uwezo wa kununua kitu chochote zaidi ya mahitaji yake ya kila siku na pesa ni za kugawiwa.Basi linasimama kwenye kituo kimoja mbele na Shuhuda rafiki yake anaingia. Shuhuda ana uzuri wa kuvutia, alivalia kipeponi na kutenda kama Wapeponi. Afida anashawishiwa na Shuhuda kufanya (kutenda) kama Wapeponi lakini anaghairi. Afida anatueleza hapendi watu wanaofuga nywele kirasta, na anaturudisha nyuma siku ya kwanza kumwona Saparata. Saparata ni mtukutu, anayesomea tamaduni za kiafrika katika Chuo Kikuu cha Peponi. Saparata humfuata Afida kila mahali akimtamani lakini hapumbaziki. Shuhuda na Afida wakati huu wanakaribishwa na Saparata kwenye sehemu ya mapumziko 'Zaman' na kununuliwa vinywaji naye. Hapa Afida anapokea simu kutoka kwa Shaabani anayemwarifu amelezwa hospitali katika chumba mahututi kutokana na maradhi ya moyo.Ujumbe huu unasababisha Afida kubogoja kitini lakini anadakwa na Shuhuda. Shuhuda na Saparata wanampeleka nyumbani kisha siku mbili baadaye anaelezwa kifo cha Shaabani na kwa miezi mitatu hakuweza kunyanyuka kitandani kwa huzuni. Bi. Marneti alikasirika sana na kumtishia kumrudisha Motoni. Anakarambuka na Bi. Marneti anamwondosha kabisakabisa nyumbani na kumpeleka chuoni kusoma kipeponi. Mienzi tisa inapita, Afida anaeleza shida za pale Taasisi ya Lugha ya Peponi. Tokea siku ya kwanza wenzake darasani wanamtenga, wengine wanambagua, naye mwalimu wa darasa hakumwamini kabisa kama angeweza kuwa na akili ya kufahamu kipeponi na pia pesa za matumizi alizoletewa na Bi. Marneti hazikutosha kamwe. Anahitimu masomo ya miezi tisa ya  lugha ya Peponi,na kupokea zawadi ya kuwa mwanafunzi wa kwanza wa Motoni kufaulu vizuri tokea miaka kumi na tano iliyopita.Usiku wa manane bwenini Chuo Kikuu cha Peponi, mwaka mzima umepita.Afida yuko kitandani anagaragara, usingizi hauji na hawezi kumudu masomo yake pia. Sauti zinaanza kupenya ndani ya ubongo wake, kumtaka adadisi usiku na mchana wa Motoni. Siku hizi anachukia sauti zile zinazomrejesha Motoni bila ya kusita kwani alishafika pahala alipopatamani siku nyingi. Anajisemea kuwa watu wa kwao mpaka sasa huwajui hana chochote anachokichuma mwenyewe, nategemea pesa za kugaiwa tu. Sauti inasema Motoni ni pahala pa balaa tupu kisha Afida anaeleza tafsiri ya usasa ambao

unaimarika na kubadilika kwa namna nyingine katika kipimo cha nukta na dakika. Kila wakati akili yake inamwambia ana haki ya kudharau maisha ya Motoni. Anakumbuka maisha yake yote, anakumbuka jinsi babake alivyokuwa ruwaza kwake;kila Alhamisi kuamkia Ijumaa yeye pamoja na watoto wa nyumbani,wa majirani na wa mitaani walivyokusanywa na babake akawasikiliza jinsi walivyoendelea kumudu kitabu kitakatifu.Vilevile udogoni alivyowafundisha Abjadi na alivyofurahia kusoma,hasa jinsi angerekebisha historia ya ubinadamu katika siku zijazo. Babake Afida anatiririkia chumbani kupitia dirisha kwa mzunguko wa sufism, akimfanya Afida kushangaa kwani miaka miwili hajaja kumzuru. Babake kwanza anamkumbusha nasaha alizompa,za kutenda na kutendana, kutenda na kutotenda. Pili dini zote zinaelekea Aheri na hakuna atakayekuwa anamjua mwenzake katika familia yao. Tatu mahubiri aliyowapa ni ukweli mtupu wa maisha na mwishoni anamfafanulia na kumwonyesha utengano wa Afida na mamake na yeye Afida hakuwa na furaha kama zamani. Mazungumzo haya yanamfanya Afida kujitathmini, anapatwa na huzuni na kuputikwa na machozi. Babake anapoondoka anapatwa na usingizi. Afida anatueleza kuhusu uhusiano wake na Yakrobich. Anakutana na Yakrobich wanapofika wiki moja kabla ya kuanza masomo ukumbini mwa Leisure Hall katika Taasisi ya Lugha Peponi anapovutiwa na muziki.Yakrobich anamnunulia chakula na soda, wanafahamiana na kucheza densi pamoja hasa wimbo wa Marvin Gay  “What’s going on?”. Uhusiano wao sasa umekua zaidi ya miaka miwili isipokuwa Afida anakataa mapenzi ya mwili naye kwani haoni kama yatamletea furaha. Yakrobich ni limbukeni wa Peponi Mashariki, mtoto wa matajiri wapya, mwenye heshima na mshindani asiyependa kushindwa.Afida anatukumbusha babake aliyekuwa kiongozi na harakati zote za dini alivyomdokezea kuhusu Sufism, umuhimu wa muziki kwa mwanadamu akimwelekea muumba wake na alivyompa uhuru usiokuwa na mipaka hadi akawa shabiki wa muziki nyumbani na mitaa ya karibu na kwao. Maisha yanamregeza na kuubaradhulisha ushujaa wa Afida hadi anaubadilisha msimamo wake. Neshboch, mzee wa miaka sitini na miwili na mpenda maisha anamgundua Afida nyumbani kwa shangaziye na kwa sababu hii anafanya sherehe nyingi nyumbani kwake ili kumteka Afida lakini anaambulia patupu, kwani kila wakati anamnyemelea kwa namma jeuri na ya kumdhalilisha. Bw. Bawa na Bi. Marneti wanamshawishi kumkubali na siku moja Afida anamkubalia usuhuba tu. Neshboch anamtembeza kwenye utajiri wake na wanakula na kunywa kwa utonofu.Yakrobich

anapongundua Afida ameimili upande wa Neshboch, anapandwa na hasira na kumwambia anajiuza na kuwaibisha vijana wote hivyo anajenga ukuta wa dharau na chuki kati yao.Bi. Marneti anayejua uhusiano wake na Yakrobich anambakulia Afida kuwa Yakrobich si rafiki bali anataka kumkandamiza tu, anamtweza Neshboch kuwa mwenye busara na faida kuliko Yakrobich kwani anaweza kumpatia uraia.Mwanga wa uhitaji wa mtu kama Neshboch unaanza kumwingia Afida na nasaha za Bi. Marneti zinamwingia nafsini, anajisabilia kwa Neshboch kabla ya ndoa kukamilika, wanapata mtoto nje ya ndoa hadi uzito huu wa mambo unamfanya Afida kuahirisha masomo kwa miaka tatu. Neshboch anampatia Afida msaada anaouhitaji katika maisha yake na ya mtoto na kulipiga chenga suala la kufunga ndoa mwanzoni lakini mwishowe anakubali na wanafanya harusi. Mfululizo wa majira unaleta kero badala ya furaha Peponi kwani mwanzoni maisha ya ndoa na Neshboch yanakuwa murua kabisa anatawazwa umalkia, pesa na neema zinamzunguka naye Dinda mtoto wao wa kiume anacheza naye na kuzungumza kuhusu maisha. Uhusiano wa Bi. Marneti na Afida unaanza kuwa mzuri anapohakikishiwa na Afida kwamba kwa vyovyote asingeingia mikononi mwa mumewe, lakini anapozaa tu! Uhusiano wao unachafuka tena anapomshawishi Neshboch na kubali kumpa mtoto wao wamlee kwani huwa tasa lakini Afida haruhusu hilo. Maovu yanazidi She-shaiza (ndugu ya Neshboch) anapoamua kumuandama kwa simango za ubaguzi. Miaka minane imepita na ndoa ya Neshboch na Afida imeshuhudia mabadiliko mengi kwani haina mashiko ya mapenzi ya kweli kwa sababu waliifunga kwa kigezo cha utajiri na uzawa wa Neshboch Peponi.Siku hii Afida anaeleza kuwa ameshapata uraia na paspoti ya Peponi na She-shaiza anakuwa mtu wa kwanza kumkejeli. Ukejeli huu unamfanya Neshboch na Bendelheib waingilie kati lakini Neshboch anatetea She-shaiza, jambo linalomfanya Afida akasirike, atoke nje na kuchukua gari, na kulitimua bila ya kumsubiri Neshboch. Anaenda kwa Profesa Marjan na mkewe Mama Maryam wanaompa mawaidha kusimama kidete na kuwaonyesha Neshboch na She-shaiza udhaifu wao kwa njia ya uungwana.Vilevile wanamfahamisha kuwa Shuhuda alikuwa amelazwa hospitalini kwa ugonjwa wa kisasa usiopona. Siku baadaye Neshboch anampiga Afida nusura amuue kama Dinda asingeingilia na baadaye anamfungia nje. Nje anawapigia Profesa Marjan na mkewe simu ili waje kumchukua na jioni ile, ndoa yao na Neshboch inafikia kikomo. Profesa Marjan na mkewe Mama Maryam ni baba na mama wa kupanga wa Afida, wanatoka nchi moja jirani ya Motoni.

Afida anakutana na Profesa Marjan Chuo Kikuu cha Peponi kwani ndiye Profesa wa mwanzo kutoka Motoni kuja kusomesha Peponi. Hawa wanamchukua kama mtoto wao, wanampa nasaha na fikra za kijiutuuzima. Afida anapewa talaka na kufukuzwa na Neshboch bila chochote. Mahakama inampa haki ya kukitunza kitoto chake na vilevile inaamuru Neshboch amtafutie Afida pahala pa kuishi na Dinda, na kudhamini gharama za kuendesha maisha ya Dinda; jambo ambalo linamkera Neshboch mno. Siku moja usiku polisi wanapigiwa simu na majirani wa Afida na kuambiwa kwamba Afida ana mchezo wa kurudi usiku wa manane katika hali ya ulevi 'topu' na anapoingia ndani amezoea kukipiga makofi ki-Dinda. Jambo hili si kweli kama polisi wanavyopekua. Lakini mahakamani hakimu anambandika jina la 'mama katili' huku wakili wake Afida akinunuliwa kwani haitetei kesi ya Afida kihalali. Afida analemewa jinsi mahakama inavyomkandamiza na kumwangusha chini kwa kumpa haki mumewe. Suala la Neshboch kumpiga vibaya vibaya Afida hadi anakaribia kufa, linageuzwa na kumfanya Afida kuwa ndiye mkosa kwa vile anamghadhabisha Neshboch kupita kiasi. Haruhusiwi kukilea kitoto chake Dinda kwa kisingizio kwamba ni Mama mlevi. Katika unyonge wa kutengwa na ki-Dinda, Afida anapoteza kabisa imani anayokuwa nayo kuhusu Peponi na pia kuupoteza mwili wake ambao hapo zamani alidhani ungekuwa wake wa kumsabilia mwanamme mmoja tu ambaye anampenda na kumheshimu, zaidi anashindwa kuzuia tabia ya kunywa pombe kwa wingi, anaingia katika mtego wa kukaribishwa ulevi na wanaume kwa mtindo wa nipe nikupe. Afida anakuwa hatoki tena kwenye baa akiwafuata wafadhili wake ambao nao wanataka kufadhiliwa. Babake anapomzuru na kumkaripia kwa kuyaharibu maisha yake, anamfukuza na kumwita maiti asiyejua chochote. Baadaye anapasua kilio, analia kwa uchungu na kuwaza kwa nini alimkubalia Neshboch kunywa pombe na kumpa mimba. Anajiwa na fikra ya kupata mtoto mwingine na anapokuwa katika baa maarufu ya 'The Lost'anakutana na Saparato; wanakunywa pombe mpaka wanakuwa hawajitambui tena na kulala kitanda kimoja nyumbani kwa Saparato. Kitoto kinachozaliwa kinaitwa Mkombozi. Kuzaliwa kwa Mkombozi kunamfanya Afida aache ulevi moja kwa moja kwani sheria ya Peponi isingeruhusu mama mlevi aachwe alee mtoto. Anapewa pesa na serikali kumhudumia mtoto, lakini hazitoshi kwa hivyo anatumia ufundi wake wa kuchonga vinyago na kufuma vitambaa vya mapambo na kuviuza. Pesa anazozipata anazitumia kama nyongeza ya zile anazopewa na serikali kumhudumia Mkombozi. Siku moja anapokuwa

akichonga kinyago anapata maumivu makali tumboni. Anaenda hospitali na kugunduliwa na saratani ya fuko la uzazi, anafanyiwa operasheni.Siku moja baadaye anapokuwa amelazwa hospitali (baada ya kufanyiwa operesheni) anajiwa na mwuuguzi wa wadi ya UKIMWI anayemwomba afike kwenye wadi kumwona Shuhuda aliye katika hatua yake ya mwisho. Afida anaenda, wanazungumza na Shuhuda hadi anaishiwa na nguvu. Miezi sita baada ya kifo cha Shuhuda, Profesa Marjan anapokea simu kutoka kwa Afida akilia kwa gugumio na huzuni, anasema anaumia na kuuliza sababu iliyomfanya mamake kutomuua wakati alipomzaa, alitumana mamake aambiwe amsamehe na amwombee kwa babake anapomtilia ubani, na mwisho anaomba asamehewe na Profesa Marjan na Mama Maryam kwani dunia ilimfikisha pabaya kisha akakata mawasiliano. Profesa anapoenda kumfuata hampati kamwe, alimwona Mkombozi pekee, akamchukua na kumwacha ndani ya mikono ya polisi. Miaka sita imepita na Profesa Marjan hajakutana na Afida na hakuna anayemwona wala kujua alikokwenda

### 2.3 Uhalisiajabu katika *Mhanga Nafsi Yangu*

Riwaya ya kimajaribio hushughulikia matatizo yanayoikabili nchi na jamii husika na kwa kiasi fulani inakiuka mipaka ya kitaifa na kimataifa hadi ulimwengu wote. Katika sehemu hii, tulionyesha maswala mbalimbali kama yalivyojitokeza katika riwaya ya *Mhanga Nafsi yangu* Pia, tunakubaliana na Mbatiah (2001:93-94:) anayesema hivi kuhusu Uhalisiajabu, "Istilahi hii inatumiwa kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo na matukio ya kifantasia husawiriwa kwa kuiga mtindo wa uhalisia, yaani kwa kuyaeleza kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida. Wasanii wanaoutumia mtindo huu hudhamiria kuonyesha kuwa ingawa mambo yanayoshughulikiwa ni ya kiajabuajabu, hutokea katika maisha ya kawaida ya jamii inayohusika." Uhalisiajabu ni njia mpya ya kuuwasilisha uhalisi unaotuzunguka katika jamii. Katika *Mhanga Nafsi Yangu*, Said. A Mohammed alijikita katika mazingira na matukio ya jamii na kujaribu kuyasawiri kwa njia mpya ya Uhalisiajabu. Kutokana na maelezo haya, tunaonelea kuwa wasanii hawautumii Uhalisiajabu kiajali, bali kwa lengo la kuangazia hali ya jamii wanamoishi. Riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ni ya kimajaribio kwani nadharia ya Uhalisiajabu imetumika ambapo matukio halisi yanayotendeka katika jamii yanawasilishwa kwa

njia mpya. Hivyo basi katika sehemu hii tumeonyesha matukio halisi ya jamii kama yalivyowakilishwa katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*.

### 2.3.1 Ubaguzi

Afida anapowasili Peponi anabaguliwa nyumbani kwa shangaziye. Chumbani alimolala mlijaa baridi na hamkuwa na vukuto la joto la kutosha ilhali wenzake walilala ndani ya vyumba vilivyokuwa na joto la kutosha. Afida alilala kwa shida kwani baridi ilimwingia mpaka mifupani mwake kila siku. Inasemekana kuwa shangaziye Afida Bi Marneti ndiye aliyemwamuru alale kwenye chumba kilichokuwa na baridi, ili azoezwe baridi huku akipelelezwa iwapo alikuwa na maradhi. Licha ya kuwa alipimwa na madaktari walioaminika. Wanapeponi, shangazi yake walimwona Afida kama mleta maradhi na kumbagua. (Uk. 30). Hali hii ya kunyimwa vuguvugu la joto chumbani mwake likimpelekea kuugua kitetemeshi cha mwili na mafua makali.

Bi Marneti alimbagua Afida pale alipomkataza kuoga. (Uk. 37). Alimkejeli kwamba hata angeoga mara mbili kwa siku asingeweza kuwa "mweupe" kama Wapeponi. Akielekea shuleni kila siku, Afida alikuwa akibaguliwa na Wapeponi. Hawakutaka kuketi karibu naye wala mazungumzo naye kwani alikuwa si mmoja wao. Abiria wengi wa- Peponi walimkodolea macho tu yaliyojaa chuki naye alikuwa akivalia sura ya tabasamu tu ili kuwadanganya kuwa hakujua kilichoendelea. Afida anakisia kuwa vitabu, redio na runinga husambaza uzushi na upuuzi mtupu kuhusu nchi za Kiafrika, nao Wapeponi wengi huziamini habari hizi bila ya kutaka kutambua sababu. Vyombo hivi vya habari hudaganya na kutia chumvi mambo mabaya kuhusu Peponi ili kutia msisimko habari zao. Afida alibaguliwa kwa kasumba kuwa, Wamotoni ni wajinga na washenzi kwa sababu waliumbwa hivyo na hawawezi kubadilika (Uk. 64).

Afida alibaguliwa kwa sababu ya mavazi yake yaliyoonekana kupitwa na wakati hasa akiwa Peponi. Shuhuda alimweleza kuwa iwapo angetaka mambo yake yatengenee kule Peponi ingebidi afuate mizani iliyotakiwa, kukiwepo kubadilisha mavazi ya Kiafrika na kuiga mfano "bora" wa Ki-peponi. Afida na Shuhuda wakizumgumzia mabadiliko haya aliyotakikana

kuyafanya Afida, Wapeponi waliokuwa kwenye basi walishangazwa na lugha hiyo iliyokuwa na kelele zilizokera. Lugha ambayo haikuwa na ustaarabu. Wanatilia chumvi kauli hii kwa kusema kuwa, Wamotoni ni watu wenye kelele na fujo kila siku.

Ubaguzi unadhihirika wazi darasani. Wanafunzi walimtenga Afida kama kwamba alitoka mwezini (Uk.90), walimwona kuwa si mtu. Mle darasani aliulizwa maswali magumu ili kujaribiwa fahamu yake iliyodhaniwa kuwa ilikuwa chini kuliko ya Wapeponi. Kupata rafiki Mpeponi ilikuwa vigumu kwa Afida kwani walimbagua na pili Wapeponi hawakuuthamini urafiki kama Wamotoni.

Ndoa ya Afida kwa Neshboch ilikumbwa na ubaguzi. Dada zake Neshboch walimbagua Afida waziwazi na hata mmoja wao (She-saiza) kumtusi kwamba yeye Afida ni kitakataka na hangefaa kupata uraia wa nchi yao takatifu. Peponi, mumewe Neshboch pia alishirikiana na dada zake kumdharau Afida eti kwa sababu ni Mmotoni (uk. 153).

Ubaguzi huu uliendelea katika ndoa ya Afida, huku mumewe, aliyejawa na kiburi na kasumba za Peponi kwamba Wamotoni hawakuwa na lolote zuri, kuishia kumtaliki bibiye Afida na kutumia sheria, iliyosheheni ubaguzi kumnyang'anya Afida kitoto chake.

Katika baa ya *The lost*, Afida anapozua rabsha kwa sababu ya ulevi, mhudumu alimfokea kuwa yeye ni mwanamke mweusi na hakufaa kamwe kupiga kelele pahala hapo kwani hapakuwa Motoni kwao.

Afida alipopata kitoto cha pili na Sapataro, babake aliyekuwa Mpeponi alikibagua na kusema kuwa hata jamii yake haingekikubali wala kukipokea kwani hakikufanana na Wapeponi. Sapataro alimdokezea Afida kuwa ilifaa atambue kwamba yeye si Mpeponi wala kitabu cha visa, au kijikaratasi hakingemfanya kuwa raia halisi wa Peponi. (Uk.185).

### 2.3.2 Ukengeushi

Waafrika wengi wanapohamia Peponi huacha tamaduni zao na kuiga Wapeponi. Bi Marneti shangaziye Afida alipokuwa Motoni alithamini utu, umoja na hakuwa na tamaa. Alipenda mapenzi safi yasiyo ya pesa, kuuthamini ukoo wake na hakuropokwa ovyo.

(Uk.51). Alipohamia Peponi, alichukua tamaduni za huko na kutupilia mbali tamaduni za Ki-Motoni hasa alipokata uhusiano na ukoo wake kiasi cha kumdhulumu Afida aliyekuwa kama mtoto wake.

Shuhuda rafikiye Afida aliyetoka Afrika aliiga Uzungu kwa mavazi, ulevi, hulka na hata lugha. Alivalia vijiguo vilivyomuacha tuputupu kama anavyodai Afida. Alivuta sigara ambayo inadaiwa kuwa haikumtoka mdomoni (Uk.71). Alienda kwenye mabaa na kushiriki ukware uliomfanya aambukizwe ukimwi. Mambo haya yote Shuhuda aliyaiga kutoka kwa Wapeponi ambapo hata Afida hakuamini kuwa ni Shuhuda aliyemfahamu kule Motoni. Shuhuda anasisitiza kuwa iwapo mwanamke yeyote anagependa mambo yake yamwendee vyema kule Peponi, hakuwa na budi ila kuonyesha mwili wake (Uk 73).

Afida alikengeuka naye kwani haikupita miaka mingi kabla abadili mienendo yake ya Kiafrika aliyoishikilia shadidi hapo awali. Aliingia kwenye ndoa yake na Mpeponi, Neshboch iliyomfanya abadilike kabisa. Aliingilia ulevi ambao baadaye ulikithiri mipaka na kumwacha bila familia. Alikesha kwenye mabaa na kusabibisha zogo kali kila alipoenda kupiga mtindi. (Uk. 181). Alianza hata kuomba mwanamume yeyote ampe mimba hadharani (uk. 181). Afida akawa hauheshimu mwili wake na kuanza kushiriki ukahaba ambao mwanzoni alidhani kuwa ni jambo lisilowezekana. Hii ni baadhi ya mifano ya wahusika waliokengeuka katika riwaya.

### 2.3.3 Umaskini

Jamii ya Kiafrika inaendelea kukandamizwa na wageni wanaotoka nchi za Magharibi. Mataifa haya ya wameyadhibiti masoko ya Motoni ambapo tunawaona wageni hawa wakija Motoni na kununua matunda kwa bei ya chini. Hii inasababisha umasikini kwa Wamotoni kwani hawafaidiki katika juhudi zao za kuzalisha mali**.**

Kuhamia kwa Afida Peponi kulikuwa na msukumo wa kuasi ulitima na kusaka mali Peponi. Tunaelezwa kuwa Motoni kulikumbwa na umasikini kiasi kwamba hakuna jambo njema lolote lililoweza kumea, kuwa au kukua katika nchi hii (Uk.3). Afida alilalamika Jinsi kule kutegemeana kwa ukoo wa Kiafrika kunavyozidisha umasikini hivi kwamba, mtu akionekana kufaulu, lazima ukoo ugawane mafanikio yenyewe hata kabila hayajazaliwa. Eti mtu akifanikiwa kidogo, anakuwa mateka wa ukoo unaomnyofoa nyama harakaharaka na kumegwa kila upande hadi mtu huyo abaki mifupa mitupu (Uk. 6). Hii ni ishara tosha kuwa Afida ametoka katika jamii iliyokumbwa na umasikini.

Katika maelezo ya Bi Sinangoa, tuanona kuwa Afida alilelewa kwa ukata kwani mara nyingi akienda kwa bibi huyu (Sinangoa) kupata angalau chakula. Wakati mwingine Afida akipata kwa Singangoa hakukuwa na chakula, bibi huyu alikuwa akimtafutia angalau visenti vidogo ili kununua chakula duni huko vijijini.

Kazi aliyoifanya Bi. Mwamda baada ya kifo cha mumewe ni ishara tosha ya umasikini. Inasemekana kuwa bibi huyu aliibeba familia yote mabegani kwa kazi ya kupika na kuuza uji wa mtama, mikate ya gole na supu ya makongoro. Juu ya hayo, alikesha kuponda maandazi na mikate ya kusukuma aliyoipeleka dukani. Ujira wake ulikuwa duni (Uk. 13). Bi Mwamda alifurahi kuwa mwanawe Afida angeumaliza umasikini huu kwa kufanya kazi Peponi. Bi Mwamda anakiri kuwa tokea kifo cha mumewe, kila kiungo cha mwili wake kilimuuma kwa mzigo aliomwachia wa kuwalea wanawe.

Umasikini unadhihirika Afida anaposhangazwa na vyombo vilivyokuwa ndani ya nyumba ya Bi. Marneti ambayo yeye mwenyewe hakuwa ameviona huko kwao Peponi. Vyombo hivi

inasemakena alivisikia tu na kuvisoma kwenye vitabu. Mwalimu wa Afida naye alidhihirisha umasikini kwani hata hangeweza kununua suti wala kufunga tai.

### 2.3.4 Madhara ya ulevi

Tatizo la dawa za kulevya ni moja kati ya matatizo makuu katika jamii zetu. Pombe ambayo inaweza kujumlishwa katika kundi panala dawa za kulevya imetumiwa kama burudani katika jamii kwa kipindi kirefu sana. Katika jamii za zama za leo, kuna shinikizo za kijamii na kitamaduni ambazo zinawafanya watu wengi kuishia kuitumia pombe au bia na kuvuta sigara. Utumiaji wake unaathiri anayehusika pamoja na jamii yake. Utumizi wa sigara umeweza kusababisha utegemezi wake kwa kiasi kwamba hawezi kutenda pasi kuitumia. Kwa mfano, tunaelezwa na Afida kuwa Miongoni mwa watu wanaoathirika kwa kiasi kikubwa na tatizo la dawa za kulevya ni vijana. Kwa nini vijana wanaathirika kiasi hiki? Utumiaji wa dawa za kulevya unawavuta vijana ambao wamo katika harakati za kuwa huru na kuusaka ujitambuaji. Baadhi yao wanaelekea kuamini kuwa dawa hizi zitawapa sifa muhimu za kujitambua kama ujasiri, kujiamini na hisia za kuwa huru. Ni katika hali hii ambapo elimu ifaayoni muhimu ili kusaidia kuwaelimisha wanaohusika pamoja na jamii nzima. Moja kati ya sababu kuu zinazochangia kuweko kwa tatizo la utumiaji mbaya wa dawa ni kuvunjika kwa muundo wa mshikamano wa kijamii ambao ni msingi muhimu sana. Ikiwa msingi huu uliotegemewa na wanajamii umevunjika, uwezekano kuwa baadhi ya wanajamii watashindwa kukabiliana na hali yao mpya. Hawa watajaribu kusaka kimbilio fulani kwenye dawa za kulevya. Hii kwao inakuwa kama njia ya kujipumbaza na kujihakikishia kuwa wanaweza kuikabili hali hii mpya. Afida anapohama anakumbana na hali ambazo hakuzizoea katika tamaduni walimokulia. Matatizo yanayohusiana na ulimbukeni huo wa maisha ya mjini unaweza kumtosa mtu kwenye dawa za kulevya. Katika kiwango cha jamaa, matumizi ya dawa za kulevya, yanauathiri ushikamano wa umoja wao. Watumiaji wa dawa za kulevya wanazongwa na kurengwa na tabia yao kiasi kwamba haja za watu wengine ndio muhimu kwao. Anayehusika anaathirika kiafya na kisaikolojia. Jamaa yake nayo inateseka kumwona mwenzao akiangamia kutokana na

kuzitegemea dawa za kulevyva. Mtumiaji aliyerengwa na dawa za kulevya huwa tayari kufanya lolote ili apate pesa za kununulia dawa hizo. Matumizi ya dawa za kulevya chuoni yanachochea kuwapo kwa matendo yanayohusishwa nayo. Matendo hayo haya ni kama wizi,ukahaba,utovu wa nidhamu.

Ulevi hupelekea mtu kutoelewana na wenzake, kutowajibika na kuonekana mjinga katika jamii. Ulevi umejitokeza wazi kupitia kwa Afida, Neshboch, Sapataro na shuhuda. Waliothirwa pakubwa na ulevi ni wanawake hawa wawili; Afida na Shuhuda. Punde tu Neshboch alipomfunza Afida ulevi, ndoa yao iliingia misukosuko. Neshboch mwenyewe alimpiga bibiye Afida bila huruma na hata kumfukuza usiku wa manane (Uk. 170).

Afida naye baada ya kutalikiana na mumewe alisingiziwa ulevi na kunyang'anywa kitoto chake Dinda. (Uk. 176). Hapo ndipo alipoamua kuwa, kwa kupagaziwa hilo jina mlevi basi hakuwa na budi kuwa mlevi halisi. Ulevi huu ulimpekelea Afida kuishiwa na pesa kwani baada ya talaka hakupata pesa zozote kutoka kwa Neshboch (Uk.176). Hata kitoto chake cha pili alikipata kupitia ulevi huu kwani aliamua kupata mimba kwa walevi wenzake huku kilabuni (Uk. 181),

Sapataro ndiye mhusika aliyekuwa akilewa na Afida kila wakati kwenye mabaa. Hakuwajibika kwa ulevi huu kwani baada ya kumpa Afida mimba aliwatoroka mama na mwanawe. Shuhuda naye kwa upande wake alikuwa mlevi wa pombe na pia sigara. Uraibu huu ulimpelekea hata kuingilia ukahaba na kuambukizwa gonjwa la ukimwi.

### 2.3.5 Uasi

Uasi umejitokeza kwa wahusika wengi hasa kwa Afida aliyeuasi ukoo wake na kukata minyororo yao huku akilalamikia kurudishwa nyuma na utegemezi wa Kiafriaka. Afida alimuasi mpenziwe Shaaban aliyemuandikia barua kila wakati tangu alipoenda Peponi. Afida naye hakujibu barua hata moja kwani anadai mapenzi yake kwa Shaaban yalikwisha (Uk.69). Peponi

ilimsahaulisha kabisa mapenzi haya ya Shaaban hata yakampelekea Shaaban kuugua ugonjwa wa moyo na kufariki (Uk.87).

Afida aliasi wazazi na walezi wake huku akisingizia kuwa alishafika alikotaka. Peponi. "Aliyeniambia nirudi nyumbani, nilimuuliza nilichokisahau nyumbani". (Uk. 105). Anaendelea kusisitiza kuwa kwao mtu ni anapoamua kuishi na kwake yeye sasa ni Peponi.

Uasi wa dini umejitokeza kwa wahusika Afida na Shuhuda ambao waliyapuuza mafunzo ya dini zao. Kwanza kabisa, katika dini yao ya Kiislamu, hawakufaa kuingilia ulevi ambao ni kinyume na maadili ya dini hiyo. Mavazi yao na pia mienendo yao huko Peponi haikuenda na mafunzo ya dini hiyo (Uk. 178). Bi Marneti naye pia aliuasi ukoo wake kwani katika sura ya pili, tunaambiwa kuwa tangu ahamie Peponi hakuwahi kurudi nyumbani. Hali hizi za uasi zinajitokeza kwani wahusika wanajaribu kuyaacha maswala ya Motoni ambayo ndio hasa yanayowafanya wabaguliwe. Kuasi utamaduni wa Kiafrika kwa Afida na Shuhuda kunawafanya waingilie tamaduni za Kipeponi ili wakubalike huko kulikojaa ubaguzi wa kirangi haa kwa jinsia ya kike.

### 2.3.5 Kukata tamaa

Wahusika waliotoka Afrika wameishia kukata tamaa. Afida akiwa Peponi majira ya baridi aliteseka sana kiasi kwamba alianza kuteta na nafsi yake. Sauti ndani yake ilisisitiza arudi kwao maana ishara za kushindwa zilikuwa wazi kwake. Alikata tamaa hata kabla hajaishi Peponi kwa muda mrefu (Uk.25). Hii ilisababishwa na ubaguzi na udhalilishaji wa Wapeponi kwa Wamotoni. Maisha ya Afida Peponi yanakumbwa na shida nyingine anapopata habari kuwa mpenziwe Shabaan amefariki. Afida alikata tamaa kimapenzi na kuamua kuwa hangempa ahadi ya mapenzi mtu mwingine yeyote.

Baada ya muda mrefu, Afida aliamua kuolewa na Neshboch. Ndoa iliyoishia kutalikiana. Afida aliingia kwenye ndoa hii ili apate uraia wa Peponi (pasipoti) na pia, alitaka kuishi maisha ya

kitajiri na furaha aliyotarajia kupata kwa mumewe. Ndoa hii ilimpelekea Afida kukata tamaa kimaisha kwani mambo yalikuwa kinyume na alivyotarajia. Neshboch aligeuka katili, mlevi na mume asiyewajibika ambaye hakuwaheshimu wanawake na hasa wanawake wa Kiafrika – aliwabagua.. Aliungana na adui zake Afida wakamtesa na kumpa talaka ambapo tamaa ya utajiri na furaha katika ndoa ilikatika.

Sheria ya Wapeponi ilimbagua Afida na kumfanya anyang'anywe kitoto chake kwa misingi isiyokuwa na ukweli wowote. Hii ilimfanya Afida akose mwelekeo wa maisha yake kabisa. Alihisi kama kwamba ameshapoteza umama wake pia. Alilia kwa uchungu na kulaani kukubalia kuolewa na Neshboch na kumzalia kitoto (Uk. 177). Aliingilia ulevi na kupata mtoto mwingine ulevini ambaye alibaguliwa na babake Sapataro kwa kisingizio kuwa na nywele nyeusi. Alikata tamaa kuolewa na mwanamume mwingine. Maisha yalipomshinda, Afida hakuonekana tena kwani kwake maisha ya Peponi yalikuwa magumu kutokana na ubaguzi uliompelekea kukta tamaa. Motoni nako hakungeendeka tena.

Shuhuda naye alikuwa haendewi na maisha vizuri. Ujana na uchangamfu aliokuwa nao ulikwisha malizwa na gonjwa la ukimwi. Alipoenda kumtembelea hospitali, Afida alishtuka kumpata katika hatua ya mwisho ya maisha yake (Uk. 187). Alikuwa kabaki gofu la mtu. Shuhuda anajuta na kuonyesha kuwa hana hamu tena ya kuishi, naye Afida anasisitiza kuwa heri wangebaki Motoni (Uk.188). Walichokimbilia Peponi hawakukiona kwani walibaguliwa na kuishi maisha ya udhalilishaji hadi wakakata tamaa.

### 2.3.6 Kasumba za Kimagharibi

Wapeponi wana kasumba nyingi kuhusu Waafrika. Wanadharau Waafrika kwa jumla na bara lao.  Katika mazungumzo yake na babake, kabla hajafariki, kila wakati Afida aliambiwa kuwa "kila kitu kibaya kimebandikizwa weusi" (Uk. 21), yaani hakuna kitu kizuri kilichopotikana Afrika.

Bi Marneti licha ya kuwa Mwafrika, aliidharau bara hili. Jambo hilo linadhihirika wazi anapomwambia daktari aliyemtibu Afida kuwa Afida ni mbumbumbu mzungu wa reli kwa mambo ya kisasa kama "heater" ambayo hayapatikani Afrika. Alikuwa akisisitiza jinsi Afrika ilivyoachwa nyuma na teknolojia na kwa jumla Waafrika wote waliathirika na ujinga huu kulingana na Bi Marneti.

Darasani wanafunzi walimkejeli Afida kwamba Waafrika wengi hawasomi na kwamba huko Afrika hakuna hata vyuo vikuu. Katika mazungumzo ya Afida na Sapataro, Sapataro alishikilia kuwa lugha ya Peponi ndiyo ngumu zaidi kuliko lugha zozote duniani .Kauli hii ilikuwa kuonyesha lugha ya Peponi ndiyo iliyokuwa bora zaidi duniani na kwamba lugha zingine zote zilikuwa duni hasa za Motoni (Uk. 91).

Yakrobich naye aliamini kuwa siasa ya Peponi magharibi ndiyo siasa pekee inayoweza kutawala dunia nzima. Yakrobich alichukia ubishi wowote na Wamotoni kwani aliwaona kama watu duni (Uk. 125). Katika safari zake Afida kwenye treni, alikumbana na watoto waliojazwa uongo kuhusu Afrika na elimu walizopewa kwamba Afrika hakuna shule hata moja. Wapeponi hudanganywa hivyo ili waone mataifa yao ni makubwa kuliko mataifa yote duniani. (Uk. 137).

Bi. She-saiza naye alidharau vyakula vya Motoni kwamba havikuwa vitamu kama vya Peponi, kwamba waafrika hunywa damu (Uk. 150), aliendeleza Kasumba zake kuwa Waafrika hula vyakula vyenye mafuta mengi sio kama Wa-Peponi waliojali uzuri wa vyakula vyao (Uk. 151).

### 2.3.7 Wasiwasi

Afida haamini kuwa anahamia Peponi licha ya kuwa kesha abiri ndege kuelekea huko. Mwandishi anatwambia kuwa Afida amepoteza mashiko ya nafsi yake na kupoteza uwezo wa kuzingatia kitu kingine chochote isipokuwa kutojiamini kuwa anaelekea Peponi (Uk.2).

Mazonge yamemjaaa Afida akilini kiasi kwamba anasahau umuhimu wa safari hii inayonuiwa kabadili maisha yake.

Safari yote hii ya kueleka Peponi Afida ana wahka hasa ndege lilipoanza kuenda mrama tunaelezwa kuwa Afida alichuchupaa kama samaki aliyebanwa nyalioni na kukaushwa motoni (Uk.4).

Wahka huu unasingiziwa kutokana na hofu kuwa Afida alikuwa anaenda ugenini, hakuwa na uhakika wa utu wa shangazi aliyemwita kwenda huku, hajui huko peponi tungemchukulia vipi? Wasiwasi huu huenda ikawa ni kiona mbele cha maisha atakayokumbana nayo huko Peponi. Afida hana uhakika na kuhama bara lao kwani tunaona akijiuliza "kitu gani kinachomfanya mtu ahame kwao alikozaliwa? Kwa nini kuna kuhama kutoka kule ambako mtu kaacha mabaki ya utoto wake yanayomkaa na kumkera siku zote akilini mwake na ambayo yatamkera hadi pale atakapokutana na kifo chake?" (Uk. 19).

Wasiwasi wa Afida unadhihirika anapokuwa mahakamani akikitetea kitoto chake. Alihofia kuwa sheria ya Peponi ingetumika kumnyang'anya mtoto. Wasiwasi huu ulimvaa hadi pale aliposingiziwa ulevi na kunyang'anywa Dinda.

Mamake Afida, Bi.Mwamda pia alikumbwa na wasiwasi Afida alipokuwa akielekea Peponi. Anahofia kuwa Afida angeisahau familia yake kama wafanyavyo Waafrika wengi wakienda Peponi. Shaaban naye anahofia mapenzi yake na Afida kufikia hatima kwa safari hii ya Afida ya kwenda Peponi (Uk 10). Bi Marneti pia amekumbwa na wahka pindi tu Afida anapoingia kwa nyumbani kwake. Hii ni kwa kuwa alimwonea wivu na kudhani kuwa angemnyakua mumewe.Wasiwasi huu unampelekea kumbagua, kumdhulumu na kumchukia Afida.

**2.3.8 Nafasi ya mwanamke na ubaguzi**

Katika uhalisia wa Peponi kulikuwa na mgawanyo wa kazi na matakwa kwa kila jinsia, wanawake walipewa majukumu kama kupika, ulezi wa watoto na shughuli nyinginezo za nyumbani, kwa mfano Afida alimlea Kisura baada ya kifo cha Sada aliyefariki, (uk. 11). Bi. Sinangoa anamwinjikia Afida chai mekoni ili apate kisabeho baada ya wazazi wake hawakuwa na senti nyekundu .Wanawake hawazungumzi mbele ya umati wala kufanya maamuzi makali ya kifamilia Afida anaonyesha haya anaposema, "Udogoni mwangu, mara nyingi niliambiwa na wazazi wangu nijizuie kujibu anaposema mtu…lazima niziweke fikra zangu ndani mwa nafsi yangu. Niziweke zisitoke nje kuja kumtusi hata anayebananga," (uk. 11). Familia mtazama msichana wao kwa karibu na kama kuna shida wanaingilia na kuitatua. Wanaume nao walitoa ulinzi, walifanya maamuzi kuhusu maswala muhimu ya jamii, na kukimu mahitaji yote ya familia kama alivyofanya marehemu babake Afida kabla ya kifo chake. Wanawake wengi kama vile Bi Mwamda (mamake Afida), Afida, Shuhuda na waliouza kwenye vyumba vya burudani usiku walibaguliwa. Bi Mwamda alifanya kazi za kijungu jiko kama vile kupika uji, mikate na mahamri kuwauzia wafanyikazi wa sulubu asubuhi huku jioni akipekeka maandazi kwenye maduka (uk. 13). Katika hali hii, mwanamke huyu anatwikwa majukumu ambayo kwa kweli si yake jambo hili hutokea mara nyingi katika familia za Wamotoni. Huu ni uonevu wa jinsia ya kike.

Kwa upande mwingine, tamaduni za Peponi zinawadhalilisha na kuwabagua wanawake ambapo wanatumiwa kama vyombo vya kujistarehesha kwa wanaume. Hili linadhihirika wazi kwa mhusika Shuhuda aliyeingilia ukahaba na kuambukizwa ukimwi. Afida naye alikuwa mkware baada ya talaka yake na hakumchagua atakayesuhubiana naye, kwake mwanamume yeyote angekuwa sawa hata kumzalisha. (Uk. 181). Wahudumu katika baa nyingi walikuwa wanawake ambao baada ya kuuza pombe na vyakula vya asusa walishiriki ukware (Uk. 181), ambao kulingana na tamaduni za Peponi, ukahaba ulikuwa jambo la kawaida tu kwa wanawake wa Motoni.

Mwanamke anatumika kumbagua mwanamke mwenzake,  Jambo hili linadhihirika wazi kupitia kwa Bi Marneti anayemgeuka Afida na kuwa adui yake mkubwa. Hii ni kwa wivu aliomuonea baada ya kupata kitoto kwani yeye alikuwa tasa. Chuki hii ya Bi Marneti ilichangia kuvunjika kwa ndoa yake. Bi She-Saiza naye anambagua Afida na kumtusi hadharani kwamba hafai kuwa mke wa ndugu yake. Alishirikiana na Bi Marneti kuchochea nduguye amwache Afida. Ubaguzi unaojitokeza

### 2.3.9 Tamaa

Katika sura ya kwanza, tunaelezwa jinsi Waafrika wengi walivyo na tamaa ya kwenda Peponi. Wengine wameishia kufa kwa tamaa hii. Mwandishi anasema kuwa, “kuna wengine wanaojaribu kukata jangwa la Sahara na kuishia kukumbwa na joto, kiu na kikausho cha maji mwilini na ambacho mara moja humpoteza mtu uhai wake”. (Uk1). Jambo hili linapelekea Waafrika kuhamia wanakobaguliwa.

Afida naye anahamia Peponi kwa tamaa ya kuyaboresha maisha yake kutoka kwa umasikini aliokuwa nao. Tamaa ya utashi inamtawala Afida anapohamia Peponi na kumpelekea kuolewa na mzee aliyemzidi umri kwa jina Neshboch. Ndoa hii haikuwa ya mapenzi ya dhati kwani Afida mwenyewe anakiri kuolewa ili apate cheti cha kuwa raia wa Peponi na kuirithi mali ya Neshboch. Tamaa hii ndio iliyomwingiza Afida katika ndoa iliyojaa ubaguzi. Tamaa ya mtoto ilimpelekea Bi. Marneti kumchukia Afida na kumbagua licha ya kuwa shangaziye. Hii ni kwa sababu Bi. Marneti alimtaka mwanawe Afida awe wake naye Afida akakataa. Jambo hili lilisababisha uhasama uliopelekea ndoa ya Afida kusambaratika kwani, Bi Marneti, Bw. Bawa na Neshboch waliungana na kumbagua Afida na kuivunja ndoa yake.

Tamaa ya anasa mtindi na usasa ndiyo iliyompelekea Shuhuda kupoteza maisha yake. Hii ni kwa sababu aliasi utamaduni wa Kiafrika na kukengeuka huku akiwaona Waafrika walioshikilia dini wakati huo kama vile Afida kuwa walikuwa wamebaki nyuma.

Tamaa ya mtoto ilimpelekea Bi Marneti kumsaliti na kumbagua Afida mtoto wa dadake. Hapo awali alimpenda kama mwanawe na kumtafutia nafasi ya kutembea na kuishi Peponi. Alimlipia hata karo na kuishi naye nyumbani kwake. Alipopata kitoto na kukataa Bi Marneti akikichukua, uhasama ulizuka na bibi huyu kufanya lolote kumdhuru Afida na kuhakikisha wamemnyang'anya kitoto.

## 2.4 SABABU ZA KUHAMIA PEPONI

Mojawapo ya sababu za kuhamia Peponi ni elimu. Elimu uhusudiwa sana sio barani Afrika tu lakini duniani kote. Hata hivyo, kasumba zilizojazwa Waafrika kwamba, maisha bora, matibabu bora, teknolojia na hata siasa nzuri hupatikana Peponi, ndivyo wanavyoamini kuwa elimu bora hupatikana huko. Lengo kuu la Afida kuhamia Peponi lilikuwa ni kusomea chuo kikuu cha Peponi. Hii ingemfanya mtu wa kutajika akirudi Afrika au akiwa huko Peponi. Bila elimu bora, ni vigumu sana kwa mtu yeyote kupata ajira nzuri. Afida alipopata mimba na kuacha shule, hakupata kazi na ndio ilipelekea kuteseka sana alipoachana na bwanake kwani hakuwa na mtu wa kuyakimu maisha yake. Profesa Marjani naye alihamia Peponi ili kujipatia elimu ya juu na baadaye akawa Profesa wa kwanza kutoka Afrika kuwahi kufunza kwenye chuo kikuu cha Peponi (Uk 157). Mama Maryam naye alihuzunika sana Afida alipopata mimba na kuacha masomo yake yaliyokuwa ndio hasa lengo kuu la Afida kuhamia Peponi. (Uk.158).

Ukosefu wa kazi umekuwa donda sugu barani Afrika. Hali hii inapelekea watu wengi hasa vijana kutojikimu kimaisha hata baada ya kupata elimu. Waafrika wengi huishia kutafuta tiketi kama vile Afida, Shuhuda, Prof. Marjan na bibiye mama Maryam wamepata ajira Peponi licha ya kuwa ni Waafrika. Katika kilabu ya *The lost* Waafrika wengi wameajiriwa kazi duni ya kuuza pombe. Hii inaashiria jinsi Waafrika wengi wanavyohamia Marekani kutafuta kazi.

Uraia wa Peponi unahusudiwa sana na Waafrika. Hii ni kwa sababu Peponi kunahusishwa na maisha mazuri, utajiri na kwa jumla kila kitu kipatikanacho huko ni bora kikilinganishwa na Afrika.Viza ni cheti apewacho mtu ili kumwezesha kuishi katika nchi ya kigeni na ni mojawapo ya sheria za uhamaji. Hii inapelekea Afida kuwasaliti marafiki wa umri wake ili aolewe na mzee Neshboch akikusudia kupata viza ya Marekani. "Maadamu, nimeolewa na Neshboch, uraia na uenyeji wa Peponi sasa ulikuwa mikononi mwangu……hati ya ndoa na hati ya umiliki wa mali wa Neshboch mara moja ziliweza kubadilisha uraia wangu kuwa wa Peponi"(Uk 146). Afida alifurahia sana kupata cheti hiki kwani sasa uwepo wake Peponi ulihalalishwa kisheria na angeishi huko kwa kipindi alichopenda, hata milele.

Waafrika wengi wanapoona maisha hayawaendei vizuri barani Afrika, hutafuta suluhu Peponi. Maisha mapya huenda yakawa ni kimapenzi, kama alivyoanzisha Afida na Neshboch, kifamilia kama alivyofanya Bi Marneti na kuachana na ukoo wake, kimazingira pale wahusika wengi wanapobadilisha mazingira yao ya Kiafrika na kuhamia kabisa katika mazingira mapya ya Peponi. Afida, Shuhuda na Bi. Marneti walifungua kurasa mpya za maisha yao na katu hawakurudi nyuma kuikumbuka Afrika. Waliuasi ukoo wao, wapenzi wao wa Motoni, na hata utamaduni wao wa Kiafrika. Kulikuwa ni kama kuzaliwa upya na kuikumbatia Peponi kama wenyeji.

## 2.5 MANUFAA YA KUHAMIA PEPONI.

Mtu anapohamia Peponi, huingiliana na kujuana na watu wa tamaduni mbalimbali, elimu na mionoulimwengu tofauti. Hii husaidia kubadilishana mawazo hasa kiusomi au katika maendeleo ya taifa au bara. Profesa Marjani ambaye ni Mwafrika anayefunza falsafa ya Afrika huko Peponi, pia amejifunza falsafa ya Peponi, ambayo pia anaifunza. (Uk 157). Kufahamu falsafa za bara hizi mbili kunafanya profesa huyu kuwa na ujuzi na mawanda mapana ya ujuzi wa falsafa. Ujuzi huu unamfanya mtu apevuke kimawazo na kuwa na muonoulimwengu mpana. Profesa Marjan na

Mama Maryam wanaishi vizuri huko Peponi kwani masomo yamewawezesha kuwa na mwingiliano mwema na Wapeponi kwani wanawaelewa vyema pamoja na tamaduni zao.

Wafanyikazi Peponi hulipwa vema kulingana na kazi wanazozifanya wakilinganishwa na wafanyikazi wa Afrika. Hii ni kutokana na ukweli kuwa nchi hizi zimepiga hatua kimaendeleo, na pia sheria za wafanyikazi zinafuatiliwa vyema zikilinganishwa na za bara la Afrika. Wafanyikazi wengi na wasomi wa Kiafrika huhamia Peponi kufanya kazi huko. Hii ni kwa sababu huwa wanatafuta mapato mema ambayo mara nyingi hayapatikani Afrika. Profesa Marjan ni msomi aliyetajika kwa falsafa ya Kiafrika na badala ya kuifunza falsafa Afrika, anahamia Peponi na kuifunza huko kwani huko mapato ni bora Zaidi kuliko Afrika.

## 2.6 MADHARA YA KUHAMIA PEPONI

Wahusika wengi walipohamia Peponi waliziacha jamii zao na hata wengine kuzisahau kabisa wasirudi tena Afrika. Tunaambiwa kuwa Bi.Marneti alipohamia Peponi na kuolewa, hakuwahi tena kurudi kwao Afrika. Alibadilisha jina na kuuasi ukoo wake. (Uk.13).

Huzuni iliyotawala kila pahali kwenye uwanja wa ndege hasa kwa Bi Mwamda akimlilia mwanawe kwamba asije akaganda na kuselea Peponi inaonyesha uchungu wa kutengana na jamii. Machozi ya Shaaban na Afida wakitengana na kuhofu kuwa mapenzi yao yamefikia hatima ya ghafla inaonyesha uchungu wa kutengana. Bi.Zaina, Bi.Sinangoa na kile kitoto alichoachiwa Afida pia walikuwa kwenye uwanja wa ndege kutengana na Afida huku kila mmoja akiwa na huzuni ya kutengana huku. Hata hivyo, kama alivyotabiri Bi. Mwamda, Afida hakuwahi kurudi tena Afrika wala kukutana na jamii yake. Aliishia kufia huko Peponi. Mapenzi yake na Shaaban yalikwisha muda kidogo baada ya kufika Peponi na baadaye akatupilia mbali ahadi alizokuwa nazo kwa ukoo.

Upweke humkumba mtu anapohamia kwenye mazingira mapya. Hali hii hutokea pale ambapo, mtu anapotengana na jamii na marafiki zake aliokuwa nao, hujipata peke yake katika bara jipya alilohamia, hasa bara ambalo limekumbwa na ubaguzi kama Peponi. Tunaambiwa kuwa, Wapeponi hawathamini urafiki kama walivyo Waafrika. Afida alipoenda Peponi, hata shangazi yake aliyempeleka huko hakuwa rafiki yake. Nyumbani alikuwa mpweke ambapo kila wakati alijifungia ndani ya chumba chake huku akiwaza na kujililia tu. Shuleni, ilikuwa vigumu sana kwa Afida kupata rafiki wa Peponi. Wote walimbagua kwa kumwona duni. Afida mwenyewe anakiri kwamba kupata rafiki wa kweli Peponi ilikuwa si rahisi. Shuhuda aliyekuwa Mwafrika mwenzake ndiye waliohusiana kirafiki. Wanaume Wapeponi waliomfuata Afida walitaka uhusiano wa kimapenzi na wala si urafiki wa kawaida tu. Baada ya kutalikiana na mumewe, Afida hakuwa na rafiki mwigine wa dhati kule Peponi. Hospitalini alikolazwa Shuhuda alikumbwa na upweke kwani hakuwa na yeyote wa kumtembelea. Jamii yake yote ilikuwa Afrika isipokuwa Afida aliyeenda kumtembelea akiwa katika siku zake za mwisho. (Uk.187).

Bara la Afrika huwa hakuna baridi kali ikilinganishwa na majira ya baridi huko Peponi. Mwafrika anapoenda Peponi hujipata katika hali ngumu ya kukabiliana na baridi hii. Tunaambiwa kuwa baridi hii inagandisha na kupekecha huku ikiathiri kila kitu vibaya vibaya. (Uk.24). Lazima mtu aweke chombo cha kutia vuguvugu la joto chumbani cha kulala ili asiathiriwe na baridi hii kali. Baridi hii kali ilimwathiri Afida kwani ilimwingia usiku alipolala na kumfanya augue kitetemeshi cha mwili na mafua. Daktari anasisitiza madhara ya baridi hii kali kwa kumtahadharisha Afida kuwa huweza kuua kwa kuharibu viungo vya mwili kabisakabisa. (Uk. 37). Baridi hii bila shaka ni changamoto kwa Waafrika wanaohamia Peponi.

Waafrika wanapohamia Peponi hukumbana na utamaduni mpya. Maadili na tamaduni za Kiafrika hutupiliwa mbali hasa dini na mavazi.Waafrika wengi huiga tamaduni za Peponi ambazo huchukuliwa kama usasa na zilizo bora. Shuhuda kwa mfano alikengeuka na kutupilia mbali maadili ya Kiafrika.Alivalia viguo vifupi na kuvuta sigara hadharani. Hii ilikuwa kinyume cha dini ya Kiislamu alikokulia Shuhuda. (Uk.74). Alienda kwenye vyumba vya starehe na wanaume tofauti huku akipiga mtindi kupindukia. Haya ni baadhi ya mambo aliyoiga Shuhuda kutoka kwa utamaduni wa Peponi. Baadaye, Shuhuda aliugua ukimwi na kufa labda kwa

kujiingiza kwa anasa za Kipeponi na kuyaasi maadili ya Kiafrika. Afida naye alijaribu kuushikilia utamaduni wa Kiafrika hadi pale alipoolewa na Neshboch. Bwanake huyu alimbadilisha kabisa Afida na kumfanya aingilie ulevi. Ulevi huu ulizidi alipopewa talaka na hata akawa kahaba wa kuzurura kwenye mabaa akitafuta wanaume. (Uk.179). Alikuwa akijiuza kwa malipo ya chupa moja tu la bia. Msichana aliyejiamini kwa uzuri wake na maadili mema alibadilika kwa kuiga uzungu ambapo alikata tamaa na kujiua hatimaye.

Mara nyingi ndoa za kigeni huwa na manufaa lakini katika riwaya tuliyoteua, ndoa tuliyoshuhudia ya kigeni imemletea Mwafrika balaa tupu. Afida alopohamia Peponi, alimuasi mpenziwe wa Afrika Shaaban na kuyasaka mapenzi huko Peponi. Hali hii ilimpelekea kuolewa na mzee wa miaka karibia sabini Bw. Neshboch. Ndoa hii ilimfanya Afida aige tamaduni za Peponi hasa zile hasi na kumkubalia mumewe kwa lolote alilotaka hata kama lilikuwa baya. Neshboch alimwingiza Afida ulevini na baadaye kamwacha kwa kumsingizia ulevi uo huo. Hii ni kwa sababu ndoa hii haikuwa na mihimili ya mapenzi ilhali ni tamaa iliyowaongoza wapenzi hawa wawili. Afida alitaka viza na maisha mazuri yautajiri, naye Neshboch alimtamani Afida kimwili. Bi. Marneti alimshawishi shangazi yake huyo kuolewa ili naye adumishe urafiki na Neshboch. (Uk.146). Kila mtu alipata alichokitamani na Afida anafurahia sana kuwa na uraia wa Peponi mikononi baada ya kupata cheti cha ndoa. (Uk.146). Hata hivyo, ndoa hii haikudumu kwani baada ya muda mrefu, Neshboch aliishiwa na tamaa zake kwa Afida na kuanza kumdharau kila wakati, na hata kukikataa chakula alichokipika. (Uk.168). Neshboch anamwambia Afida hadharani kuwa uchu wake kwake ulimwisha na kumwomba talaka (Uk169), huku akimchapa na kumuumiza kila mara. Baadaye wakaachana na Afida kunyang'anywa mwanawe Dinda. Kusambaratika kwa ndoa hii kulikuwa pigo kubwa kwa Afida kwani maisha yake mazuri na utashi wa Peponi zilifika kikomo. Kutokana na mfano huu, ndoa hizi za kigeni zimesawiriwa kama zisizofaa na zenye maafa yake.

## 2.7 SABABU ZA UBAGUZI

Mtu akijiamini na kujipenda, ataamini na kuwapenda watu wengine pia. Wanaobaguana huwa na tatizo hili la kisaikolojia kwamba, wageni wakikaribishwa huenda wakawanyang'anya wenyeji kazi, vyeo, ardhi na pia uongozi. Hali hii inapelekea visingizio na vikwazo wanaomwekea Mwafrika ili wazidi kujiona bora Zaidi. Hata hivyo, Waafrika wengi wanaohamia Peponi huwapiku wenyeji kwa mambo mengi hata kuwafanya wawe na wivu. Mfano mzuri ni pale Afida anapoibuka wa kwanza katika masomo ya lugha chuoni na kuwashinda Wapeponi wengi. Wapeponi wote walimwonea Afida wivu isipokuwa Yakrobich ambaye ndiye peke yake aliyemfurahia Afida. (Uk.96). Hii ilieneza chuki zaidi kwa Wapeponi kwani Afida alizidisha kutojiamini kwao.

Ubaguzi husababishwa na watu kutoelewa na tamaduni, dini na maadili ya wengine .Hii hutokana na watu kuwa na mionoulimwengu finyu na hasa kushikilia misimamo hasi kuwahusu watu wengine. Elimu ya Peponi aghalabu haiwapi wenyeji taswira kamili ya nchi za Motoni. Vyombo vya habari vya Peponi navyo huegemea upande wa maovu ya Afrika badala ya kuonyeshana na uzuri pia. Watu wengi ambao huwa hawajishughulishi kupata ukweli wa mambo hushikilia uongo huu usio na mashiko nakutoelewa kwao kunasababisha ubaguzi. Wahusika waliojazwa uongo huu ni kama vile She-Shaiza ambaye alionyesha ujinga wake hadharani alipoanza kuyazungumza mambo ya kijinga kuhusu Afrika mbele ya watu wengi kwenye hoteli. Alidai kuwa Waafrika hula na kupendelea vyakula vyenye mafuta ilhali kwenye sahani lake alijaza kipande cha nyama ya nguruwe (Uk 151). Hii inaonyesha kuwa, ubaguzi unaweza kusababishwa na kutozielewa tamaduni, maadili na itikadi za watu wengine.

## 2.8 MADHARA YA UBAGUZI

Ubaguzi husababisha anayebaguliwa na anayebaguana kutokuwa na mkabala mwema. Afida alipobaguliwa na vile vitoto vilivyotoka shuleni alijawa na chuki sana kwani vilimkejeli yeye na elimu ya Kiafrika. Abiria waliokuwa kwenye basi na Afida walimtazama kwa chuki naye aliwapa tabasamu la kudanganya (Uk 63). Moyoni alielewa chuki ya hao abiria hasa bibi mmoja aliyezoea kupanda naye basi lilo hilo kila siku, kwamba ilikuwa ya kubaguliwa yeye kwani hakuwa Mpeponi. Chuki ilisheheni hata shuleni alikoenda Afida kwani alidhaniwa kuwa na fahamu ya chini kuliko wanafunzi wote waliokuwamo darasani. (Uk.90). Anasisitiza kuwa wanafunzi walimtenga na kumuona dude tu. Ilimwia Afida vigumu kupata rafiki na alidai kuwa, "Mpeponi huwa rafiki yako tu pale anapokuwa na haja, akishapata alichokitaka huwa tena si rafiki yako". (Uk.90). Chuki hii ilifanya hata darasani wasijadiliane na kusaidiana kimasomo.

Uhusiano baina ya Bi. Marneti na Afida ulijaa chuki na kufanya wawili hawa wawe maadui wakubwa. Afida alibaguliwa kwa wivu aliokuwa nao Bi. Marneti kwa mumewe akihofu kuwa Afida angemnyakua bwanake. (Uk.39). Chuki hii ilipelekea Bi Marneti kumwondoa Afida nyumbani na kumpeleka kusoma lugha ili asionane na mumewe.

Chuki baina ya mwenye baa ya *The Lost* ilisababishwa na ubaguzi. Mwenye baa alimtusi kwa kumwita 'mwanamke mweusi' na kumwonya kuwa hiyo baa haikuwa Afrika. (Uk.81). Uhasama huu wa kurushiana maneno hadharani ulimalizwa na Sapataro alipowatenganisha wahusika hawa. Chuki baina ya Neshboch na Afida ilisababishwa na ubaguzi. Neshboch alimchukia Afida kuwa yeye si Mpeponi na kumwambia kuwa alikuwa amemwokota jaani na hakuwa na budi kumwacha. Afida alitalikiwa na kunyang'anywa kitoto chake. Jambo lililomkatisha tamaa na kupelekea kifo chake.

Ubaguzi husababisha upweke hasa kwa anayebaguliwa. Waafrika wengi wanapohamia ugenini hujipata bila familia wala marafiki ndiposa inawabidi watafute familia na marafiki wapya. Katika hali hii, mtu hujihisi mpweke hasa anapoanza kubaguliwa. Nyumbani kwa Bi. Marneti, Afida anakumbwa na upweke kwani mara nyingi tunampata kwenye chumba alichotengewa

akijililia peke yake. Anapowapata Bw. Bawa na Bi. Marneti wakigombana sababu yake, hakuwa na yeyote wa kuzungumza naye angalau amtulize isipokuwa kulia kwa kwikwi na kekefu chumbani mwake.( Uk 43). Upweke huu ulimzidi hadi akaanza kujizungumzia. Aliomba kiumbe chochote kile kisimame mbele yake aseme nacho. (Uk 44).

Upweke ulimzidi Afida shuleni kwani alisema kuwa alitamani kuwa na rafiki Mpeponi ili angalau amsaidie akipatikana na shida kule. Alitamani kuwa na mtu ambaye angemlinda na kumtetea iwapo angepatwa na tukio lolote lile. (Uk 90). Hata hivyo, hakuna aliyekuwa radhi kuwa rafiki yake kwani kama alivyodai Afida, Wapeponi hawakuuthamini urafiki kama walivyokuwa Waafrika na aliishia kuambulia upweke pale shuleni.

Ndoa ya Afida ilimwondolea upweke kwa muda lakini ubaguzi ulipoingia, Neshboch aliupiga teke uhusiano wao na upweke ukamtawala Afida hasa baada ya kutalikiwa. Bi. Marneti naye alishirikiana na Neshboch kumnyang'anya Afida mwanawe wa pekee. Alibaki bila yeyote. Upweke huu ulimpelekea kuwa mlevi ashiki na pombe ikachukua nafasi ya marafiki. Ikawa rafiki yake wa dhati. Aliingilia pia na ukahaba. (Uk 180) na baadaye kuyaharibu kabisa maisha yake. Haya yote yalisababishwa na ubaguzi hasa ulipomwingia mumewe.

Upweke ulizidi hospitalini alikolazwa Shuhuda. Ijapokuwa Shuhuda aliugua kwa muda mrefu, hakuwa na yeyote wa kumtembelea na kumliwaza kule hospitalini. Hii ni kwa sababu marafiki wale aliokuwa nao Wapeponi walimwachia gonjwa la ukimwi na kumtoroka. Alimtumana Afida kwa miezi mingi hadi iliposadifu Afida akajipata akitibiwa katika hospitali alikolazwa. Hapa, Afida alimpata Shuhuda katika dakika zake za mwisho na kulia kwa kwikwi huku akimhurumia rafiki waliokuwa na usuli mmoja wa Afrika. (Uk.185).

Ubaguzi husababisha kuharibika kwa uhusiano mwema ambao ungekuwa na manufaa kwa wahusika. Kama tujuavyo, umoja ni nguvu katika kila sekta ya maendeleo. Wanafunzi wanapombagua Afida darasani, hawakujua kuwa angeibuka mwanafunzi bora zaidi shuleni. Wangeungana na kushirikiana naye, angewasaidia kuimarisha masomo yao lakini walipombagua, hawakufaidi chochote kutoka kwa mwanafunzi bora zaidi shuleni.

Uhusiano wa Bi. Marneti na Afida ulikuwa mwema kabla hajatoka Afrika. Hata hivyo, uhusiano huu haukudumu na ubaguzi ulimfanya mtu na shangazi yake kutengana na kuwa maadui wakubwa. Bi. Marneti asingembagua Afida, angeishi naye kama mwanawe na hata hangemwaribia Afida ndoa yake. Isitoshe, Afida angebaki na kitoto chake na wote kuishi vyema kama mtu na shangazi yake.

Urafiki ambao ungeimarisha maisha ya Afida na Neshboch ulikatizwa na ubaguzi. Uhusiano huu ungeendelea vyema na ungejenga familia yenye furaha lakini kwa kutoshirikiana, ndoa ikavunjika kwa sababu ya mume kumbagua mkewe na kumwona duni.

Uhusiano baina ya Afida na Sapataro ulikatizwa kwa sababu ya ubaguzi. Baada ya kumtunga Afida mimba ya pili, Sapataro alimtoroka hadi walipokutana kisadfa (Uk 184) akiwa na kitoto hicho.Baada ya kukikagua kitoto kile, Sapataro alisema kuwa hata wazazi wake hawangekikubali kwa sababu kilifanana na Waafrika na hakikufanana naye Mpeponi. (Uk 185). Uhusiano baina ya mtoto na babake ukakatizwa kwa sababu ya ubaguzi. Afida na Sapataro wakaachana wasionane tena. Bila shaka uhusianao huu ungezaa matunda na kuanza familia nyingine mpya ingekuwa si kwa sababu ya ubaguzi.

Afida hakuwahi kupata utulivu wa kiakili kwa muda wote huo alioishi Peponi. Kila wakati alionekana kuwa na wasiwasi kuhusu maisha kuanzia mwanzo wa safari yake kuelekea Peponi hadi hatima yake kule Peponi. Hii ilimpelekea hadi wakati mwingine kuzungumza peke yake hasa chumbani mwa Bi. Marneti walipokuwa wakizozana. Hata ingawa alizungumza peke yake, ndani ya nafsi yake mlikuwa na sauti mbili zilizozozana. Sauti moja ikimwonyesha uzuri wa Motoni na sauti nyingine kumwonyesha uzuri wa Peponi na kumwacha Afida katika hali ya wasiwasi. Hakuwa na uamuzi wowote juu ya sauti hizo mbili wala hakujua ni yapi yalikuwa maisha mazuri kwake yeye. Wakati mwingine alifikiria juu ya maisha yake na kujuta sana bila kujua alichokililia. (Uk.54).

Alipoipoteza ndoa na kitoto chake cha kwanza kwa Neshboch, Afida aliingiwa na mawazo mengi na kuingilia ulevi kabisa ambao ulimkausha pesa alizokuwa nazo. Ukosefu huu wa pesa

nao ukampa mawazo zaidi hadi akaingilia ukahaba, jambo ambalo hakuwahi kulifikiria maishani ili aweze kuyamudu mahitaji yake. Kivuli cha babake pia hakikumpa utulivu. Kila wakati kilimtokea na kuyakejeli maisha aliyokuwa ameyachagua Afida huko Peponi. Wakati mwingine kivuli hiki kilimtokea na kumwambia hivi. "Hii ndiyo ile Peponi uliyoitazamia, hukuwa hivi Afida, tulikufunza ukafunzika.Tulikuonya utosheke na chochote kidogo au duni ulichokipata, tulikusafisha ukasafishika. Sasa umekuwa nani? , umeyaharibu maisha yako". (Uk 177). Maneno haya yalimfanya Afida kuwaza zaidi na kupatwa na huzuni moyoni. Alisema kuwa utashi ndio uliomtia hatarini huku akipiga kelele kama punguani.

Mateso haya ya kisaikolojia yanamkumba Afida zaidi anapomtembelea rafiki yake Shuhuda kwenye wadi. Alimpata akikaribia kufa na kumhurumia sana huku akizungumza peke yake na kujuta kuhamia Peponi. Akafumba macho na kukumbuka ujana wake na Shuhuda. Tangu siku hiyo Afida alikata tamaa ya maisha labda kwa kuona hatima mbaya ya maisha ya rafiki yake. Matatizo haya ya kisaikolojia ambayo chanzo chake ni ubaguzi, yalimfanya Afida kujiua na kumwacha mwanawe wa pili chini ya ulinzi wa serikali. (Uk.191).

## 2.9 HITIMISHO

Katika sura hii, tumeonyesha mtiririko wa matukio kwa kuangalia muhtasari wa riwaya kwa jumla. Kwa kutathmini jamii, tumeonyesha kuwa jamii inayozungumziwa ya Afrika imekumbwa na ukata na ndio unaochangia hamu yao ya kutaka kuhamia Peponi.Kwa mujibu wa nadharia ya Uhalisiajabu, miujiza iliyomo kwenye uyakinifu wa kila siku imeelezwa moja kwa moja. Matukio haya yameelezwa kwa ukawaida tu na bila shaka mwandishi akafanikisha kazi hii ya *Mhanga Nafsi Yangu* kwa kutumia mbinu za uandishi kama vile ndoto, uzungumzi nafsia, na pia kumchora mhusika wa kiajabu anayeishi hata baada ya kifo. Mipaka ya wakati nayo inavunjwa kwani matukio hayafuatani moja kwa moja kama inavyotarajiwa katika ulimwengu halisi, mbinu ya kumbukizi imetumika pakubwa Afida anapokumbuka wosia aliompa babake akiwa angali hai.

Waafrika kama wanavyowakilishwa na wahusika kama vile Afida na Shuhuda wanafikiri kuwa suluhu za matatizo wanayokumbana nayo Afrika zinapatikana Peponi. Riwaya hii inaeleza wazi kuwa, kinyume na matarajio yao, Peponi kuna shida zake ambazo zinaonekana hata kuzidi za Afrika. Jamii ya Peponi imejaa ubaguzi wa rangi na Waafrika wanaohamia huko hawapewi nafasi nzuri kuyaendeleza maisha yao. Hali hii inapelekea Waafrika wanaohamia huko kuishia kukata tamaa na hata kufa.Wengi wao, kama Afida na Shuhuda wanajuta na kutamani kurudi nyumbani. Sababu za kuhamia Peponi, manufaa na madhara yake pia yameangaziwa. Pia, tumeshughulikia swala la ubaguzi, sababu zake pamoja na madhara yake. Hii ni kwa sababu wahusika wanaobaguliwa wote walihamia Peponi kwa sababu mbalimbali na wanakumbwa na matatizo mengi ukiwepo ubaguzi.

# SURA YA TATU

## MASUALA YANAYOWAATHIRI WANAOBAGULIWA KATIKA RIWAYA YA *MHANGA NAFSI YANGU.*

### 3.1 UTANGULIZI

Sura hii inayaangazia masuala yanayowaathiri wanaobaguliwa katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ambayo kwa njia moja au nyingine yanachangia swala hili la ubaguzi. Masuala haya ni kama vile, magonjwa sugu, ndoa za kigeni, haki na sheria pamoja na mitazamo isiyo ya ukweli ya Waafrika kuhusu Peponi. Masuala haya yanachangia ubaguzi kwa njia tofauti. Kwa mujibu wa nadharia ya Uhalisiajabu, masuala haya yanahusisha kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu. Hali mbalimbali kama uhalisi na ndoto, kifo na uhai, usasa na uzamani, shamba na mjini, ugeni na utamaduni zinaingiliana. Kadhia hizi walizokumbana nazo wahusika katika riwaya ndizo tunazoziangazia katika sura hii.

### 3.2 MAGONJWA SUGU YANAYOCHANGIA UBAGUZI

Magonjwa ni mojawapo ya vikwazo dhidi ya maendeleo ya jamii kwani pesa nyingi hutumika katika matibabu na yanayouathiri utendakazi wao. Baadhi ya magonjwa hayo ni kama vile saratani na UKIMWI ambayo ni tishio kubwa ulimwenguni. Mtu anapougua magonjwa haya aghalabu hubaguliwa hasa wahusika tunaokumbana nao katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu.*

#### 3.2.1 SARATANI

Saratani ni aina ya ugonjwa unaoanzishwa na seli za mwili zinazoanza kujigawa na kuongezeka bila kusita. Ukuaji huu unaleta uvimbe mwilini unaozidi kuwa mkubwa hadi unabana viungo vya mwili kama neva, mishipa ya damu, ubongo, mapafu, maini na utumbo. Kuna aina mbalimbali

za saratani: ngozi, mdomo, damu, figo, mdomo, fuko la uzazi, koo, matiti na macho. Visa vya saratani vimeongezeka katika jamii ya sasa. Shirika la afya ulimwenguni inaeleza kuwa watu milioni kumi na nne ulimwenguni, walikuwa wameathiriwa na Saratani kufikia mwaka wa 2012. Katika mwaka huo, vifo milioni nane ulimwenguni vilitokana na Saratani. Takwimu zinaonyesha kuwa visa vya maambukizi ya Saratani vitaongezeka kwa asilimia sabini katika miongo miwili ijayo. Visa vipya, elfu mia sita, vya Saratani vimeripotiwa katika mataifa ya Afrika, Marekani ya Kati na Marekani Kusini. Riwayani, tunasimuliwa:

"Siku moja alipokuwa akichinga kinyago alipata maumivu makali tumboni. Alipokwenda hospitali na kufanyiwa uchunguzi na daktari aligundulikana na saratani ya fuko la uzazi. Haraka alifanyiwa operesheni huku Mkombozi akienda kuwekwa katika nyumba ya malezi ya watoto wasiotakiwa na wazazi wao"… (Uk.185). Dondoo hili linadhirisha kuwa ugonjwa wa Saratani ni hatari kwa maisha ya binadamu. Afida anaumia sana hadi anajuta kuzaliwa kwani alibaguliwa na kutengwa na mtoto wake kwa ugonjwa huu. Huenda Afida aliupata ugonjwa huo kutokana na tabia yake ya kunywa pombe kwa wingi. Hatima yake haijulikani, na mwanawe Mkombozi analazimika kukosa malezi yake. Katika jamii, wanawake wengi wanaathiriwa na kansa ya mapafu, uzazi, tumbo na matiti na watu wengi wasiouelewa ugonjwa huu kwa kukosa kuhamasishwa au kutokana na mitazamo hasi kuhusu magonjwa haya huishia kuwabagua waathiriwa.

### 3.2.2 UKIMWI.

Riwayani, Afida anapomtembelea mama Maryam, anafahamishwa kuwa Shuhuda amelazwa hospitalini kutokana na ugonjwa wa kisasa usiopona. Maneno ya Maryam yanashadidiwa na kifo cha Shuhuda baada ya kuwa kwa wodi ya UKIMWI kwa muda mrefu. Katika jamii yetu ugonjwa wa UKIMWI unatambuliwa kwa semi mbalimbali. Kuna wale wanauita 'mdudu', 'sindano' au 'uchawi'.

Kuna changamoto nyingi sana zinazoambatana na ugonjwa wa UKIMWI. Ni jambo la kusikitisha unapopatikana na virusi vya UKIMWI. Baadhi ya watu wanakataa kuzikubali hali zao na kuwalaumu wengine kwa kutowaonya. Pia, wanajuta kutokana na maisha yao ya awali yanayochangia wao kuathiriwa. Afida anapomtembelea Shuhuda hospitalini, Shuhuda anamweleza: "Kwa nini hu…kunika-taza? .... hatimaye nafikwa na balaa kama hii…Labda tungebaki nyumbani…Si-jui-na-dhani tu…tu…tuliuendekeza ujana wetu…La, ujana wetu ndio uliotuponza…Ni…sa…me…he wewe". (Uk 188-189).

Maneno haya ni dhihirisho kuwa Shuhuda anapopatikana na ugonjwa wa Ukimwi anajuta kutoka kwao Motoni hadi Peponi kwani baada ya kuugua aliepukwa na kila mtu na hakukutokea yeyote wa kumtembelea hospitali isipokuwa siku ya kufa kwake alipokutana naye Afida, jambo lililotokea kisadfa. Anaonelea heri wangebaki kule Motoni ili wasifikwe na balaa yoyote. Anasisitiza kuwa ujana wao ndio unawaponza na kuwatendekeza. Anamwomba Afida msamaha na hatimaye anaaga dunia. Katika jamii ya sasa, unyanyapaa dhidi ya wagonjwa wa UKIMWI bado upo. Hata hivyo, elimu kwa umma kuhusu ugonjwa huo inaendelezwa. Aidha, waathiriwa wanaisha maisha marefu kutokana na matumizi ya dawa za kupunguza makali yanayotolewa mahospitalini bila malipo.

## 3.3 NDOA ZA KIGENI ZINAVYOATHIRIWA NA UBAGUZI

Ndoa inastahili kujengwa kwa misingi ya upendo, uaminifu na heshima. Hata hivyo, ndoa za kisasa hasa ndoa za kigeni zinakumbwa na migogoro mingi ukiwepo ubaguzi. Migogoro hii inatokana na ukosefu wa mapenzi ya dhati na mawasiliano hafifu pamoja na kutofautiana kitamaduni na kimaadili baina ya wanandoa

### 3.3.1 KUTOPENDANA KWA DHATI NA KUBAGUANA

Matheka (2014) anaeleza kuwa baadhi ya sababu zinazowasukuma watu kuoa na kuolewa ni mbaya. Watu wengi wanajitosa katika ndoa kwa lengo la kuziridhisha tamaa za nafsi zao. Mapenzi ya dhati ni nadra katika jamii ya kisasa. Wanandoa wengi wanayajenga mapenzi kwa msingi wa mali. Mapenzi ya aina hii yana misukosuko mingi. Riwayani, tunaelezwa kuwa ndoa baina ya Bw. Bawa na Bi. Marneti haijengwi katika msingi wa mapenzi ya dhati. Bi. Marneti anaamua kuolewa na Bw. Bawa kwa sababu ana mali. Afida anapofika Peponi, Bi Marneti anamwona kama adui katika ndoa yake. Anaona kana kwamba Afida anamnyang'anya mume wake. Wanapogombana na mume wake. Bi. Marneti anaona kama Afida anamnyang'anya. Bi. Marneti anamshurutisha mume wake wampeleke Afida katika Taasisi ya Lugha mbali na Peponi ili asiivunje ndoa yao. Bw. Bawa anakubali ili kumfurahisha mke wake.

Ndoa nyingine inayojengwa katika msingi wa mali ni ya Neshboch na Afida. Afida anakubali kuolewa na mzee wa miaka sitini na miwili kutokana na ushawishi wa shangazi yake, Bi Marneti. Bi. Marneti anamweleza Afida: "Nataka upate mtu mwenye kipato, lakini mwenye moyo wa kutoa…Yule aliye mzee mwenye busara…Yule mwenye sauti ya kukuweka Peponi maana ana mali nyingi. Utapoomba uraia hapa mambo mengi yatafikiriwa si darizeni ya miaka uliyokaa hapa tu, lakini nani ambaye atakuwa arbabu wako, yaani nani atakayechukua dhamana kwako, yule atakayekubali kutia saini fomu utakayotakiwa uijaze". (Uk 144). Kutokana na dondoo hili tunaona athari za ukosefu wa mapenzi ya dhati katika ndoa. Afida anaona kuwa ndoa yake ina misukosuko mingi kwa sababu anasukumwa na ubinafsi kuolewa na Neshboch. Anautamani utajiri wake na uraia wa Peponi. Anaeleza kuwa ndoa nyingi za kisasa hazina mapenzi ya kweli ndiposa zinakumbwa na migogoro. Afida anapitia dhiki nyingi kama vile kupigwa, kutukanwa na kudhalalishwa na mume wake. Hatimaye, Neshboch anaamua kumtaliki Afida. Wingi wa talaka unatokana na watu kuwa na matarajio mengi ya kibinafsi ambayo ni vigumu kutimizwa katika ndoa zao. Changamoto zinazodhihirika katika ndoa hii, zinashuhudiwa katika ndoa za jamii ya sasa. "Akili yangu iliniambia maadamu nishazaa naye, haina haja ya kunikimbia na kuniacha mweupe, kwani kuzaliwa kwa mtoto huyu nilihisi ni waraka wa hidaya ya siri ambayo isingebanduliwa milele". (Uk 147) . Dondoo hili linadhihirisha kuwa Afida

anapata mtoto nje ya ndoa kimakusudi ili aweze kumteka Neshboch. Ana matumaini kuwa Neshboch angeshurutishika kumwoa kwa sababu ya mtoto wao. Katika jamii ya kisasa, wanawake wengi hupata ujauzito nje ya ndoa kimakusudi ili kuwanasa wanaume. Baadhi yao wanafaulu kuolewa na wanaume hao ilihali wengine wanaambulia patupu. Hata hivyo, wanapooana kwa sababu ya mtoto anayezaliwa nje ya ndoa wana majuto kwa sababu ya ukosefu wa mapenzi ya dhati. Afida anapoolewa na Neshboch anajawa na majuto mengi. Anaeleza: "Duru za majira na hali ya hewa ndani ya miaka minane zimeshuhudia mabadiliko mengi ndani ya ndoa yangu. Ndio kwanza nijue kuwa maisha ya ndoa yamejaa vitimbi na mabadiliko sawa na majira ya hali ya hewa. ..Lakini ndoa yangu haikuwa tofauti na ndoa nyingine. Ndivyo zilivyo ndoa zote, na zaidi yangu ambayo haina mashiko ya mapenzi ya kweli ambayo pia ni tofauti kubwa za ratili za waliofunga ndoa ya mhanga: mhanga wa nafsi yangu na mhanga wa nafsi ya Neshboch kwa utajiri na uzawa wake wa Peponi". (uk 153) .

Mwanzoni mwa ndoa ya Afida, kuna mapenzi ya dhati. Neshboch anampenda na kumpa kila kitu anachokihitaji; magari, mavazi, vyombo vya kisasa, vyakula na vitu vya thamani. Muda unavyoendelea, ndivyo wanavyozidi kuzoeana na ndivyo ukweli kwamba amemwoa Mmotoni unavyozidi kumsumbua. Anaanza kumbagua mkewe kwa misingi hii ya rangi. Afida anapigwa, anadhalalishwa na hatimaye anapewa talaka. Katika jamii zetu tunashuhudia kuvunjika kwa ndoa kutokana na ukosefu wa mawasiliano baina ya wanandoa.

### 3.4 HAKI NA UBAGUZI

Haki ni kitu au jambo ambalo mtu anastahili kupata. Katiba ya Kenya (2010) imeangazia haki mbalimbali za makundi maalumu ya watoto, vijana, wazee, walemavu, wafungwa, wafanyakazi na wakimbizi. Tunaangazia namna watoto wanavyobaguliwa kwa kunyimwa haki zao.

Watoto wana hadhi maalumu katika jamii na ni jukumu la familia na serikali kuwaelimisha na kuwalinda. Haki za watoto kama vile malezi bora, kulindwa dhidi ya dhiki, kupewa elimu, kutofanyishwa kazi nzito na kupewa matibabu. Mara nyingi watoto hubaguliwa kihaki kwani

wengi wao hawawezi kuzitetea kutokana na umri wao mdogo na pia kutozielewa haki hizi. Tutaangazia jinsi haki hizi za watoto zinavyokiukwa na kuzingatiwa riwayani.

Mama na baba mtoto wana haki sawa katika kulinda na kuyakidhi mahitaji ya mtoto. Kila mtoto ana haki ya kulelewa na wazazi halisi au wazazi mbadala iwapo wazazi wake halisi hawajimudu kihali, kiafya au wameaga. Hakuna mzazi anayefaa kujitenga kwa vile mtoto ni wa wote. Katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*, msimulizi anakiangazia kisa cha Kisura aliyeachwa yatima baada ya mama yake kufa kutokana na ugonjwa wa UKIMWI (Uk 11). Afida anajitolea kuwa mzazi mbadala wa Kisura baada ya kifo cha mama yake. Hili linampa Kisura nafasi ya kuyafurahia maisha ya utotoni mwake.Hapa, haki ya Kisura ya malezi bora ilitekelezwa na Afida.

Mkombozi, mwanawe Afida, analazimika kulelewa na wazazi mbadala baada ya mama yake kuathirika kiafya: "…alipokwenda hospitalini na kufanyiwa uchunguzi na daktari na kugundulikana na saratani ya fuko la uzazi. Haraka alifanyiwa upasuaji huku Mkombozi akienda kuwekwa katika nyumba ya malezi ya watoto wasiotakiwa na wazazi wao kwa muda hadi mpaka Afida atoke hospitalini. (uk 185) . Afida anapojifungua mtoto, shangaziye, Bi. Marneti anamshawishi ampe mtoto wake amlee. Afida anakataa kwa sababu hukutaka mtoto wake alelewe na mwanamke mwingine akiwa hai. Afida anamlea mtoto wake na kumpa mapenzi ya dhati. Anasema:

"...Dinda hakuwa mwana tu, bali kiambata cha nafsi yangu ya nje na ndani.

Alikuwa mwenzangu katika michezo mbalimbali ambayo mwana alicheza na mamake. Pia alikuwa kiambata changu katika utukutu, uchangamfu na burudani, kicheko na hata ulinzi pia". (Uk.162).Katika usemi huu, tunaelezwa kuwa watoto huwapa wazazi wao furaha. Afida anamwona Dinda kama kiungo muhimu katika maisha yake. Wanacheza pamoja na anamjaza furaha wakati wote. Hataki kutenganishwa na mtoto wake kwa vile anajua kuwa angesalia katika upweke na huzuni. Pia, anaamini kuwa Dinda ana haki ya kulelewa na wazazi wake halisi kwa vile wangali hai. Kwa hivyo, Bi. Marneti, hakuwa na haki ya kuwa mzazi mbadala wa Dinda.

Suala la watoto kuzaliwa nje ya ndoa linashuhudiwa katika jamii ya kisasa. Sheria inaeleza kuwa watoto wanaozaliwa katika ndoa au nje ya ndoa wana haki sawa. Kila jamii ina mitazamo tofauti kuhusu watoto wanaozaliwa nje ya ndoa. Katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*, Afida anaeleza: “Wakati huu ilinijia miko ya Motoni kuhusu mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa. Afanywe nini mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa...Kwa vyovyote vile, mimi nilitaka nimpende mwanangu, nimlee, nimkuze katika nyonda za umama ili aongoke katika dunia hii ngumu, kwani umama una rutuba ya mafanikio kwa mtoto wake. Huku Peponi kwa bahati, utata huu umepungua. Mtoto kama huyu anatarajiwa kulindwa kwa kila hali”. (Uk 164)

Katika dondoo inabainika kuwa ni mwiko kumzaa mtoto nje ya ndoa kule Motoni ilihali Wapeponi wanaliona kama jambo la kawaida. Watoto wanaozaliwa nje ya ndoa kule Peponi wanapendwa na kutunzwa vyema. Afida anampata Dinda nje ya ndoa na anampenda, anamlea kwa upendo na kumwandaa vyema kuyakabili maisha ya ulimwengu wa sasa.

Mtoto mwingine wa Afida, Mkombozi anazaliwa nje ya ndoa. Baba yake, Sapataro, hawajibiki katika malezi yake. Serikali inampa Afida pesa za kugharamia mahitaji ya Mkombozi ila hazitoshi. Kwa hivyo, inambidi kutafuta pesa za ziada kwa kuviuza vinyago na vitambaa. Kutowajibika kwa Sapataro ni ukiukaji wa haki za watoto. Ni jukumu la kila mzazi kuwajibika katika malezi ya mtoto wake awe amezaliwa ndani au nje ya ndoa.

Watoto wana haki ya kuishi katika mazingira yasiyohatarisha maisha yao. Ni jukumu la wazazi na serikali kuhakikisha kuwa mazingira wanamoishi watoto yana utulivu na amani. Mazingira yaliyo na fujo na migogoro huathiri ukuaji wa watoto kiakili na kitabia. Watoto huiga na kuyatilia maanani yale yanayotendwa na watu wazima. Migogoro katika ndoa ya Afida na Neshboch inamwathiri mtoto wao, Dinda. Wanapopigana, anajaribu kumwokoa mama yake kutokana na ukatili wa baba yake kwa kumng’ata mguu. Neshboch hapendezwi, kwa hivyo anamlaani na kumfukuza. Dinda anakosa uaminifu kwa wazazi wake hasa kwa mama yake. Anamwona kama kiumbe duni kwa vile yeye ni mwanamke.

Watoto wanafaa kutengwa na wazazi ambao wanahatarisha maisha yao. Sheria ya Peponi haikumruhusu mama mlevi kumlea mtoto katika taathira ya ulevi. Afida anatenganishwa na mtoto wake Dinda, kwa madai ya kuwa mlevi. Mama mlevi anachukuliwa kama mama katili ambaye anayahatarisha maisha ya mtoto wake. Wanajamii wanafaa kuwajibika katika kuhakikisha kuwa kila mtoto anaishi na wazazi waadilifu. Hata hivyo, babake Dinda hakuwa mwadilifu licha ya kukabidhiwa haki ya kuishi na Dinda.Sheria ilitumika kumbagua Afida na kumnyima mwanawe.

Visa vya ukiukaji wa haki za watoto vinafaa kuripotiwa kwa polisi au mashirika yanayotetea haki za watoto. Haki zinapokiukwa, sheria hutumiwa kuwaadhibu wakiukaji.

## 3.5 SHERIA

Sheria ni kanuni zinazotungwa na jumuiya fulani kama vile bunge, manisipaa, jiji au jamii fulani ili kuratibu shughuli za jumuiya inayohusika pamoja na adhabu pindi kanuni hizo zikikiukwa. Hata hivyo, sheria zinaweza kutumiwa kutekeleza ubaguzi. Kila nchi ina sheria zake ambazo huiongoza katika shughuli zake za kila siku. Kila mwananchi anapaswa kuzizingatia sheria hizo ili kujiepusha na mkono mrefu wa sheria. Kuna sheria zinazoongoza sekta ya uchukuzi. Hizi zinafaa kuzingatiwa ili kupunguza ajali za barabarani. Wakiukaji wa sheria hizi wanapaswa kuchukuliwa hatua kali. Ukiukaji wa sheria za barabarani kule Peponi unachukuliwa kama kosa kubwa na wakiukaji wanaadhibiwa vikali.

Hali ni tofauti kule Motoni kwa vile askari wanapenda kuchukua hongo kutoka kwa madereva wanaokiuka sheria za barabara na kuwawachilia huru, hali hii inaleta ubaguzi kwa wasio na uwezo wa kutoa hongo kwani ndio pekee wanaoathiriwa. Mwandishi anakiangazia kisa cha Neshboch anapoendesha gari akiwa mlevi. Afida anaogopa kwa vile anajua kuwa polisi wangemkamata na kumchukulia hatua kali. Visa vya ukiukaji wa sheria za barabarani vinashuhudiwa katika jamii. Kuna dereva wanaoendesha magari wakiwa walevi. Wengine huzipuuza alama na taa za barabarani. Hali hii inachangia kuongezeka kwa ajali za barabarani.

Ndoa za kisasa zinakumbwa na changamoto nyingi. Boss (1988) anaeleza kuwa ndoa za sasa si mahali salama pa kujisitiri maana malengo ya wanaofunga ndoa ni tofauti na matarajio yao makubwa kuliko yanayoweza kukidhiwa na wenzao. Matarajio yanapokosa kutimizwa, wanandoa wanaamua kutengana. Talaka katika jamii ya sasa ni jambo la kawaida. Kalume (2013) anaeleza kuwa utafiti unaofanywa katika kaunti ya Lamu unaonyesha kuwa ndoa hazidumu zaidi ya miezi sita. Hili linatokana na kutoelewana baina ya wanandoa. Kulingana na sheria za nchi nyingi, wanandoa wanaooana kupitia kwa harusi, iwe ya kanisani au kwa mkuu wa sheria, sharti watengane rasmi kupitia mahakama. Katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* tunaelezwa kuwa Afida anapopewa talaka na Neshboch, mahakama inampa haki ya kumlea mtoto wake, Dinda. Neshboch anaamuriwa kumpa Afida makazi na pesa kumtunza Dinda.

Hata hivyo, sheria za Peponi zinawabagua Wamotoni. Hukumu ya kesi ya kugombania mtoto kati ya Neshboch na Afida inampendelea Neshboch kwa vile ni Mpeponi. Msimulizi anasimulia:

Siku ile ya hukumu, Afida alipata nguvu ya kuipeperusha imani ya Peponi iliyoganda akilini mwake kabla hata hajaingia Peponi. Sasa anaelewa kwamba Peponi sivyo ilivyofikiriwa kuwa ni pahala pa kuramba asali na kukoga maziwa na kulala kwenye vitanda vya dhahabu. Suala la sheria ambayo daima Afida alidhani ingekuwa na uadilifu, sasa alijua kuwa sheria ya Peponi ilikuwa ya upendeleo wa kijinga kwa kutegemea nani kamshtaki nani, nani ana rangi gani, na kuliko yote nani ana uwezo wa namna gani (ubaguzi). Katika kesi yake na Neshboch kwa mfano, Afida aliemewa jinsi mahakama ilivyomkandamiza na kumwangusha chini na kumpa haki Neshboch. Suala la Neshboch kumpiga vibaya akakaribia kufa liligeuzwa kumfanya Afida kuonekana kuwa ndiye mwenye kosa kwa vile alimghadhabisha Neshboch kupita kiasi. Na kama hilo halikutosha basi alipewa pigo kubwa zaidi la kutoruhusiwa kulea kitoto chake Dinda. …..Mambo yalifanywa kwa kisingizio kwamba yeye Afida alikuwa mlevi asiyestahiki kupewa dhamana kulea kitoto kile…” (Uk 171). Dondoo hili linabainisha kuwa sheria ya Peponi inawalinda Wapeponi na kuwakandamiza Wamotoni. Afida anasingiziwa ulevi na kunyanganywa mtoto wake. Kichapo alichopewa na Neshboch kilitupiliwa mbali. Afida anashtumiwa kwa kumtusi Neshboch kwa vile matusi hayo ndiyo yanamchochea kumpiga. Ni

hali ya kusikitisha kwa sababu Afida hakutendewa haki kwa vile alikuwa Mmotoni. Katika jamii nyingi, wenye nafasi hutumia sheria kujilinda na kuwanyanyasa wanyonge.

## 3.6 MITAZAMO ISIYO NA UKWELI YA WAMOTONI KUHUSU PEPONI.

Hali duni katika mataifa mengi ya Afrika huwasukuma watu kwenda katika nchi za kigeni kutafuta riziki. Nchi za kigeni zinawavutia wananchi wengi kwa sababu zina miundo misingi ya kisasa. Wainaina (2014) anaeleza kuwa kuna Wakenya wengi ambao wanapendelea kufanya kazi ugenini kuliko nchini. Hii ni kwa sababu wanavutwa na mandhari ya kuvutia ya ugenini wanayoyaona kupitia kwa vyombo vya habari au kusimuliwa na wenzao wanaowatangulia. Hata hivyo, wanapofika kule wanakaribishwa na mazingira ya ubaguzi na dhuluma kutoka kwa wenyeji. Baadhi ya Wakenya wanaofanya kazi katika nchi ya Saudi Arabia wanakufa na wengine kupotea. Majanga haya yanawafika kwa sababu hakuna sheria ya kuwalinda wanapokuwa ugenini. Katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*, tunaelezwa kuwa Wamotoni wengi haswa vijana wanatamani kufika Peponi. Tamaa hii inawasukuma kujaribu mengi ilimradi wafike kule. Msimulizi anasimulia:

"Kuna wengi wanaojaribu kukata jangwa la Sahara na kuishia kukumbwa na joto, kiu na kikausho cha maji ya mwili ambacho mara moja huweza kumpotezea mtu uhai. Baadhi, hata hawaonekani milele kwani mifupa yao hufunikwa na mchanga na kamwe hakuna anayejali. Wengine kujipakia mashuani kukabiliwa na dhoruba na mawimbi ya bahari ya Atlantiki na bahari ya Hindi. Wanaopanda magari walikwama njiani kungojea mwisho wa maisha yao. Wanaoupiga mguu hupambana na kadhia za hatari na aibu. Lakini Afida kabahatika kuwa yuko hewani". (uk1)

Katika dondoo hili tunaelezwa kuwa vijana wengi wanavumilia dhiki nyingi njiani wanapokuwa wakielekea Peponi. Wanaotembea kwa miguu wanakufa kutokana na ukosefu wa maji. Wanaoabiri meli wanalazimika kuvumilia dhoruba kali ya bara Hindi na Atlantiki na wanaoabiri

magari wanakwama njiani na hatimaye wanakufa. Kwa hivyo, Afida anajiona mwenye bahati kuabiri ndege kwenda Peponi, mahali ambako vijana wenzake hawakubahatika kufika.

Taswira halisi ya Peponi inadhihirika wakati ambapo Afida anatua Peponi. Msimulizi anasimulia: "Jibu la masuala haya, lilibainika punde pale Afida ulipomfunukia weupe kule chini baada ya lile ndege kufanikiwa kupenya yale mawingu meusi na kuingia katika uwazi na mwanga na uwazi. Sasa kila kiu kikikuwa cheupe. Ardhi nyeupe. Miti na vigogo na matawi meupe. Mapaa ya nyumba na majumba meupe. Barabara nyeupe. Mito na maziwa meupe. Weupe weupe, weupe…na weupe maana yake nini kama si weupe? Hasa ukitofautishwa na weusi? Kwani weupe si sitiari ya usafi na unadhifu wa kila mtu? Si ishara ya mafanikio. Si ishara ya Peponi kuingia kwenye fanaka na ukamilifu wa mambo ya kidunia? Si afueni na kuwemo katika ubora wa kila hali?  Afida alichanganyikiwa na masuala hayo. Hakuwa na jibu hata moja la masuala haya!" (uk 23).

Katika dondoo hili, Motoni panafananishwa na mawingu meusi yanayoleta giza duniani. Hii ni ishara kuwa panachukuliwa kama mahali duni pasipotamanika na yeyote. Kwa upande mwingine, weupe wa Peponi unaashiria mafanikio na ukamilifu wa maisha. Wamotoni wanajiona duni kwa sababu ya rangi yao nyeusi wakilinganishwa na Wapeponi weupe. Mtazamo wa Wamotoni kuihusu Peponi unawafanya wawe na matarajio mengi kutoka kwa yeyote anayebahatika kufika kule. Afida anapewa maagizo mengi na jamaa zake wakimuaga katika uwanja wa ndege. Bibi yake Afida, Bi. Zaina, anataka amletee tiketi ya ndege akatiwe meno kule Peponi. Vilevile, anamsihi amletee dola mia tano ili atie bati kwenye banda lake. Shangazi yake, Bi Sinangoa, anamweleza amtengenezee safari ya kwenda kule Peponi akapate matibabu ya tumbo. Kisura anaomba aletewa pipi. Mama yake Afida, Bi. Mwamda, anamwomba amnunulie gari moja la kubeba mizigo na basi moja la kufanya biashara ya kupakia abiria. Mchumba wake, Shaabani, anamsihi asiyasahau mapenzi yao na kizuu cha baba yake Afida, kinamkumbusha kujilinda mwenyewe. Hata hivyo, Afida anapofika Peponi anagundua kuwa hali sivyo anavyotarajia. Peponi hapampi furaha na utulivu ila anakaribishwa na majira ya baridi shadidi yanayoifanya damu yake igande. Anaiona baridi hiyo kama ishara ya karaha badala ya raha anayoitarajia. Hili linatokea pale ambapo Afida anakaribishwa na mazingira ya ubaguzi na

udhalilishaji. Shangaziye, Bi. Marneti, ndiye wa kwanza kumbagua na kumdhalalisha. Anamlaza katika chumba cha baridi licha ya kujua athari zake. Afida anapatwa na homa ya baridi inayompa maumivu makali. Aidha, anamsingizia kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mume wake, Bw, Bawa. Sauti ya ndani ya Afida inamwambia kuwa furaha ya binadamu haijakamilika kwa sababu ya utashi wa pesa na wingi wa vitu, vifaa na bidhaa. Hata hivyo, Afida anaamini kuwa Motoni kuna tamaa ila sauti yake ya ndani inampinga na kueleza kuwa Motoni hakuna utashi mkubwa wa vitu kwa sababu pesa hazipo na vitu vyenyewe havipo kwa wingi kama kule Peponi.

Pesa na vitu vinaleta mshawasha na matarajio ndani ya roho ya binadamu popote pale alipo.Wenye pesa hununua vitu kwa mchezo tu. Nguo inayonunuliwa leo haivaliwi kesho, gari kumi haziwatoshi na wao wanaishi katika nyumba za kifahari. (Uk 46- 47)

Shangaziye Afida, Bi. Marneti, anapofika Peponi anajawa na tamaa ya vitu na pesa. Sauti ya ndani ya Afida inamwambia:

"Unajua wewe…ingelikuwa si utashi wa pesa na wingi wa vitu, vifaa na bidhaa, furaha ya binadamu ingekamilika hapa duniani". (uk 45) . Kauli hii inadhihirisha kuwa furaha ya binadamu haikukamilika kwa sababu ya tamaa ya kutaka kuwa na vitu, vifaa na pesa nyingi.

Binadamu wanapokosa vitu hivyo wanakwazika na kuhuzunika. Sauti hiyo inasisitiza kuwa Bi. Marneti anatamani vitu vingi ili furaha yake ikamilike. Katika jamii tunashuhudia visa vya watu kukosa furaha kwa sababu ya kukosa pesa au vitu. Afida anapofika Peponi anataka vitu vingi zaidi ili kukamilisha furaha yake. Pesa anazopewa na shangazi yake, Bi. Marneti hazimtoshi. Jambo hili linamtia hofu kwa sababu hakuweza kuzima tamaa ya vitu iliyojaa moyoni mwake. Afida anaamua kujitosa katika ulimwengu wa anasa ilimradi apate pesa za kuuzima mshawasha wa tamaa katika nafsi yake. Hii inampelekea Afida kujiingiza katika mazingira ya ubaguzi hasa katika ndoa yake. Katika jamii ya *Mhanga Nafsi Yangu*, tunawaona wanaohamia Ulaya wakijawa na tamaa ya pesa na mali. Utashi huu unawasukuma kutupilia mbali maadili na tamaduni za kiafrika na kujiingiza katika harakati zinaowafanya wabaguliwe.

### 3.7 DAWA ZA KULEVYA

Tatizo la dawa za kulevya ni moja kati ya matatizo makuu katika jamii zetu na wanaoshiriki mara nyingi hubaguliwa badala ya kupewa ushauri nasaha. Pombe ambayo inaweza kujumlishwa katika kundi pana la dawa za kulevya imetumiwa kama burudani katika jamii kwa kipindi kirefu sana. Katika jamii za zamani na za leo, kuna shinikizo za kijamii na kitamaduni ambazo zinawafanya watu wengi kuishia kuitumia pombe au bia na kuvuta sigara. Utumiaji wake unaathiri anayehusika pamoja na jamii yake. Utumizi wa sigara ulisababisha utegemezi wake kwa kiasi kwamba Shuhuda hangeweza kutenda lolote pasi kuitumia. Kwa mfano, tunaelezwa na Afida kuwa Miongoni mwa watu wanaoathirika kwa kiasi kikubwa na tatizo la dawa za kulevya ni vijana. Kwa nini vijana wanaathirika kwa kiasi hiki?  Utumiaji wa dawa za kulevya unawavuta vijana ambao wamo katika harakati za kuwa huru na kuusaka ujitambuaji.

Baadhi yao wanaelekea kuamini kuwa dawa hizi zitawapa sifa muhimu za kujitambua kama ujasiri, kujiamini na hisia za kuwa huru. Ni katika hali hii ambapo elimu ifaayo ni muhimu ili kusaidia kuwaelimisha wanaohusika pamoja na jamii nzima badala ya kuwabagua.

Moja kati ya sababu kuu zinazochangia kuweko kwa tatizo la utumiaji mbaya wa dawa ni kuvunjika kwa muundo wa mshikamano wa kijamii ambao ni msingi muhimu sana. Ikiwa msingi huu uliotegemewa na wanajamii umevunjika, uwezekano kuwa baadhi ya wanajamii watashindwa kukabiliana na hali yao mpya. Hawa watajaribu kusaka kimbilio kwenye dawa za kulevya. Hii kwao inakuwa kama njia ya kujipumbaza na kujihakikishia kuwa wanaweza kuikabili hali hii mpya. Afida anapohama anakumbana na hali ambazo hakuzizoea katika tamaduni walimokulia. Matatizo yanayohusiana na ulimbukeni huo wa maisha ya mjini unaweza kumtosa mtu kwenye dawa za kulevya. Katika kiwango cha jamii, matumizi ya dawa za kulevya, yanauathiri ushikamano wa umoja wao.Watumiaji wa dawa za kulevya wanazungwa na kurengwa na tabia yao kiasi kwamba haja za watu wengine ndio muhimu kwao. Anayehusika anaathirika kiafya na kisaikolojia. Jamii yake nayo inateseka kumwona mwenzao akiangamia kutokana na kuzitegemea dawa za kulevya na aghalabu kumtupilia mbali.  Mtumiaji aliyerengwa na dawa za kulevya huwa tayari kufanya lolote ili apate pesa za kuzinunua dawa hizo. Matumizi

ya dawa za kulevya chuoni unachochea kuwapo kwa matendo yanayohusishwa nayo. Matendo hayo ni kama vile; wizi, ukahaba pamoja na utovu wa nidhamu ambao unasababisha mhusika kubaguliwa na watu wengine kama vile Shuhuda na Afida walivyobaguliwa.

### 3.8 HITIMISHO

Sura hii imeangazia masuala yanayowaathiri wanaobaguliwa kama vile mitazamo isiyo ya ukweli kuihusu Peponi, haki na sheria, magonjwa sugu, ndoa za kisasa na dawa za kulevya. Tunatambua kuwa Wamotoni wengi kama vile Afida, Bi. Marneti na Shuhuda wanasukumwa na utashi wa vitu na pesa kutoka kwao Motoni hadi Peponi. Watu wa Motoni wana matarajio makubwa kuhusu Peponi. Wanapaona kama mahali patakatifu palipojaa ufanisi. Suala hili linadhihirika katika jamii yetu. Tunabainisha kuwa Wakenya wengi wanaenda kufanya kazi katika nchi za kigeni kama vile Saudia ili kujiinua kimaisha. Hata hivyo, wanapofika kule wanakaribishwa na mazingira ya ubaguzi, mateso na hata kuuwawa. Ubaguzi huu unawafanya wahisi kudunishwa na kudhalalishwa. Kwa hivyo, wanalazimika kukengeuka kimaadili na kijamii ili waweze kujitambulisha kama wenyeji wa nchi hizo. Wamotoni wanapofika Peponi wanatambua kuwa Wapeponi si waadilifu inavyodhaniwa. Hii ni kwa sababu wanazikiuka haki za watoto na hakuna usawa katika utekelezaji wa sheria dhidi ya wakiukaji kwani sheria zenyewe zinatumika kutekeleza ubaguzi. Magonjwa ya UKIMWI na Saratani ni janga la kitaifa na kimataifa. Visa vingi vya maambukizi ya magonjwa haya vinaripotiwa kote ulimwenguni. Vilevile, ndoa za kigeni zinakumbwa na changamoto nyingi kwa sababu ya ukosefu wa mapenzi ya dhati na mawasiliano hafifu baina ya wanandoa, mambo ambayo yanatokana na ubaguzi. Tamaa, ubinafsi na ubaguzi zinachangia katika kuziporomosha ndoa riwayani.

# SURA YA NNE

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 4.1 UTANGULIZI

Katika sura hii, tumetoa muhtasari wa matukio kutokana na uchunguzi wetu. Tunakusudia kubainisha iwapo madhumuni ya utafiti wetu yameafikiwa. Pia, tumepima maswali ya utafiti wetu pamoja na kutoa mapendekezo ya tafiti za baadaye kuhusiana na mada yetu. Tumeeleza changamoto za utafiti pia.

### 4.2 MUHTASARI

Utafiti huu unaongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu ambayo inasisitiza kuuwasilisha ukweli kama ulivyo katika jamii kwa njia ya kimaajabu. Uhalisia na ndoto vimechanganyika kama inavyoonekana kwa mhusika mkuu. Mhimili unaosisitiza kuwa mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa huvunjwa umezingatiwa kwani maswala yanayojadiliwa riwayani yanahusu ulimwengu mzima hasa swala la ubaguzi, Wakati pia umepanuliwa kiasi kwamba tunaelezwa maisha ya mhusika hata baada ya kifo (Babake Afida). Mhimili unaosisitiza kuwepo kwa mvunjiko katika usimulizi hivi kwamba matukio hayatokei kimantiki umejitokeza riwayani kwani kuna matumizi ya mbinu rejeshi, na pia mhusika mwenye nafsi mbili (Afida). Mazingira ya kuogofya kama vile kizuu cha babake Afida ni mojawapo ya mihimili ya Uhalisiajabu ambao umezingatiwa. Utafiti huu unafanywa maktabani. Makala na vitabu mbalimbali yanasomwa ili kupata data faafu kuhusu mada ya utafiti.

Kazi hii inawasilishwa kwa sura nne. Sura ya kwanza inashughulikia suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia pamoja na mbinu za utafiti.

Sura ya pili inaangazia kutathmini jamii ya *Mhanga Nafsi Yangu*. Utafiti huu umebainisha kuwa jamii hii imekabiliwa na maswala kama vile ubaguzi, ukengeushi, umasikini, ulevi, uasi, kukata tamaa pamoja na wasiwasi wa maisha, sababu za ubaguzi pamoja na madhara yake. Pia, sababu za kuhamia Peponi pamoja na manufaa na madhara yake zinaangaziwa katika sura hii. Sura ya tatu inachunguza maswala mengine katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* yanayochangia ubaguzi. Masuala mengine ni pamoja na mitazamo isiyo halisi ya Wamotoni kuihusu Peponi, haki na sheria, magonjwa sugu na ndoa za kisasa.

Masuala haya yanatukia katika nchi mbili, yaani; Motoni iliyo Afrika na Peponi iliyo nje ya Afrika (Ulaya). Hili ni dhihirisho kuwa riwaya hii imevuka mipaka ya kitaifa hadi mataifa ambayo ni mojawapo ya teneti za nadharia ya Uhalisiajabu.

Sura ya nne ni hitimisho la utafiti. Hitimisho limetoa muhtasari wa kila sura. Maelezo yanatolewa kulingana na malengo ya utafiti. Hatimaye sura hii inaeleza matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti, matatizo ya utafiti na mapendekezo ya utafiti zaidi yanatolewa.

### 4.3 MATOKEO YA UTAFITI

Utafiti huu ulilenga kuyatimiza malengo mawili.

Lengo la kwanza lilikuwa ni kujadili swala la ubaguzi, jinsi Waafrika wanavyobaguliwa ughaibuni pamoja na madhara ya ubaguzi.

Utafiti huu umebainisha kuwa Waafrika wamebaguliwa Ughaibuni kirangi, kilugha, katika elimu na pia kitabaka. Sababu za kubaguliwa ni; kasumba za kimagharibi, Wapeponi kujiona bora kuliko Waafrika, kutojiamini na kutojuana. Madhara ya ubaguzi yamebainika kama vile chuki, upweke, kutoshirikiana pamoja na mateso ya kisaikolojia.

Lengo la pili ni kujadili kwa kina sababu za Waafrika kuhamia Ulaya na jinsi masuala yanayohusiana na ubaguzi katika jamii ya mwandishi. Imebainika kuwa Waafrika wengi

wanahamia Ulaya kwa sababu hizi: Umasikini, elimu, uhitaji wa kazi, kutafuta uraia, kuanza maisha mapya pamoja na kuikomboa jamii. Wageni wanabaguliwa katika nchi za kigeni kwa sababu ya rangi na asili yao. Ubaguzi unawafanya watu wengi kujichukia na kujidharau. Said. A Mohamed anaibua suala hili ili kuonyesha kuwa watu wote ni sawa licha ya tofauti zao za rangi, lugha, tabaka, maumbile, elimu na asili.

Utafiti huu umebainisha kuwa watu wanabaguliwa wanapougua magonjwa sugu kama vile ugonjwa wa saratani ambao ni tishio kubwa katika jamii ya kisasa. Saratani tunayoiangazia ni ile ya fuko la uzazi. Saratani haina tiba ila kuna matibabu ya kutuliza makali kama vile upasuaji na kemo. Pia, tumetambua kuwa hali ya UKIMWI ulimwenguni imedhibitiwa licha ya waathiriwa kubaguliwa kama vile Shuhuda aliyekosa mtu wa kumtembelea hospitalini. Hata hivyo, mzigo wa kuwalea mayatima ungali mzito kwa wanajamii. Kwa hivyo, kuna tahadhari ya kujiepusha na tabia zinazochangia kuenea kwa magonjwa hayo kama vile uasherati, ulevi na uvutaji sigara.

Ukiukaji wa haki za binadamu wanaobaguliwa umebainika katika jamii. Ndoa za kigeni zimekumbwa na ubaguzi na pia sheria za Wapeponi zinatumika kuwabagua Wamotoni. Watumizi wa dawa za kulevya wanabaguliwa badala ya kuelekezwa. Kwa hivyo, maswali ya utafiti yamejibiwa katika utafiti wetu ambapo tulikusudia kueleza watu wanaobaguliwa, wanaowabagua na misingi wanayotumia kubaguana. Pili, tumeeleza kwa kina sababu za kuhamia Peponi.

## 4.4 MCHANGO WA UTAFITI

Kutokana na utafiti huu imebainika kwamba fasihi hususan riwaya inaweza kutumiwa kuyaangazia masuala halisi katika jamii kama vile swala la ubaguzi. Mtunzi wa riwaya teule amejikita katika ukweli unaotokea katika jamii mbili husika; jamii ya Wamotoni na ile ya Wapeponi. Anazungumzia maswala yanayotokea wakati huu yanayohusu hali halisi ya maisha ulimwenguni kote. Masuala hayo ni kama vile ubaguzi, mafarakano katika ndoa, mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili, uchafuzi wa maadili, ukiukaji wa haki za binadamu, na magonjwa

kama saratani na UKIMWI. Utafiti huu unaielimisha jamii kuhusu vyanzo na athari za masuala hayo. Kwa hivyo, wanapokumbana nayo au kukutana na wahusika wanayoyapitia wanaweza kuyakabili. Kupitia kwa utafiti huu wanajamii wataadilika na kuupinga uovu katika jamii. Walimu wa shule za msingi na upili watanufaika katika ufundishaji wa maudhui ya ubaguzi pamoja na masuala ibuka kama inavyopendekezwa katika silabasi mpya.

**4.5 MATATIZO YA UTAFITI**

Utafiti huu umekumbwa na matatizo yafuatayo: Kwanza, kuna vitabu vichache vya Kiswahili vinavyoeleza kuhusu swala la ubaguzi, na Uhalisiajabu. Kwa hivyo, mtafiti amelazimika kusoma vitabu na makala ya Kingereza, kisha kuyatafsiri hadi kwa Kiswahili na hii inachukua muda mrefu kulingana na muda uliotengewa utafiti huu. Pili, ni vigumu kuwapata waandishi wa kazi teule ili kuwahoji kuhusu masuala mengi riwayani wanayoibua kuhusiana na ubaguzi. Matatizo mengine ni kuwa swala letu la ubaguzi halijapata suluhu mwafaka katika utafiti huu na hivyo basi linabaki kuwa tatizo katika ulimwengu wa sasa.  Hata hivyo, utafiti umekamilika.

**4.6 MAPENDEKEZO**

Utafiti huu umeshughulikia swala la ubaguzi katika *Mhanga Nafsi Yangu*. Tunapendekeza utafiti zaidi wa ubaguzi katika vipera vingine kama vile tamthilia, hadithi fupi na mashairi ya kisasa. Changamoto zinazowakumba Waafrika Ughaibuni hasa ubaguzi zinafaa kutafutiwa suluhu la kudumu. Utafiti huu umetumia nadharia ya Uhalisiabu kulibainisha suala la ubaguzi riwayani.

Tunapendekeza utafiti wa suala hilo kwa kutumia nadharia ya uhalisia. Aidha, tunapendekeza utafiti zaidi kuhusu mbinu za kifasihi na mitindo ya lugha katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*.

# MAREJELEO


Banton, Michael. (1990) *Racial Theories.* New York: Cambridge University Press.

Berkeley. (1983). *The Anatomy of Racial Attitudes*. California: University of California Press.

Gatimu, L.N. (2011). "Umenke na Ubaguzi wa Kijinsia katika Methali na Vitendawili vya Kiswahili". Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004). Nairobi: Oxford University Press.

Kimani, N. na Wafula, R.M (2009) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Magaju, J. (2004). "Uhalisiajabu katika riwaya ya Babu Alipofufuka (2001) ya S.A Mohamed na *Bina-Adamu!* (2002) ya K.W Wamitila". Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi. Standard Textbooks Graphics &Publishers.

Mdee, J. S., Shafi, A., Kiango, J.G. & Njogu, K. (2009). *Kamusi Kamili ya Kiswahili*.

Nairobi. Longhorn Publishers

Mirikau, S.A (2011). "Taswira ya mwanamke katika Tamthilia za Wamitila". Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Onyango, Oluoch (1990). "The Treatment of Racism in the works of Ayi Kwei Armah". Tasnifu ya Uzamili katika chuo kikuu cha Nairobi.

S.A. Mohamed. (2012) *Mhanga Nafsi yangu*. Tanzania: Longhorn Publishers.

Simpson, George and Eaton. (1985). *Racial and Cultural Minorities: An Analysis of Prejudice and Discrimination.* New York: Platinum Press.

Sigelman, Lee Welch, Susan (1994). *Black Americans view of Social Inequality*. Cambridge University Press.

Wamitila, K.W (2002) *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake*.Nairobi: Phoenix Publishers limited.

______________________ (2003) *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus publication.